SportPesa
TZS. 710,494,580
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**KESI YA SABAYA**

**Shahidi** adai alitishiwa maisha asipotoa milioni 90/-

UKURASA 3



**Pepe aingia rada za Milan**

UKURASA 22

Jumatano Novemba 24, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580774

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



# Samia amtwisha zigo IGP Sirro

- **Amtaka** aeleze sababu askari kuomba kupangwa Bandari au trafiki... *Ukurasa 2*



## Tanzania yapokea dozi 499,450 za chonjo ya corona

UKURASA 3



## Msuya asema marekebisho Katiba katu hayaepukiki

UKURASA 2

**MICHEZO** **MORRISON AONYESHA UUNGWANA YANGA** UK.20 **MAONI, KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan akipata maelezo kuhusu matumizi ya barabara na madaraja pamoja na kuvuka katika maeneo hayo kutoka kwa watoto wa shule mbalimbali mkoani Arusha, alipotembelea mabanda ya maonyesho kwenye maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani, katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha jana. Kulia ni Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Sirro. **PICHA: IKULU**

# Samia amtwisha zigo IGP

**Na Waandishi Wetu,**
ARUSHA

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameshtukia 'dili' linalochezwa na baadhi ya askari polisi wanaomaliza mafunzo kutumia nguvu kubwa kufanya ushawishi ili wapangwe kazi katika Kikosi cha Usalama Barabarani na Bandari.

Kutokana na hali hiyo, amemwagiza Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali (IGP) Simon Sirro, kuchunguza na kutoa maelezo ni kwa nini kuna mtindo huo na nini kilichojificha katika vikosi hivyo watu kukimbilia kupangwa.

Rais Samia alionyesha kutofurahishwa na utaratibu huo, alipokuwa akizungumza jijini hapa jana, wakati wa uzinduzi wa maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani Kitaifa, ambayo inafanyika kuanzia jana hadi hadi Novemba 28, mwaka huu.

"Kwa upande wa afande (Wilbroad) Mutafungwa (Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani) suala ni kwamba askari wengi wanapomaliza mafunzo yao, kuna 'lobbying' kubwa (ushawishi) na maombi kwa ajili ya kupangwa kwenye Kikosi cha Usalama Barabarani.

"Unajiuliza kwani kuna nini huko? Kwani askari hawezi kulobby na kuomba wapangwe kwenye malindo ya viongozi kwa mfano? Au waombe kupangwa kwenye malindo mengine. Anaomba aende trafiki au aende bandari. Unajiuliza kuna nini huko? Sasa IGP hebu kaa na wenzio, uje kunipa jawabu kwamba kuna nini huko," alisema.

"Mimi nilishawahi kuona vijana wamemaliza mafunzo, vijana wa kijijini kwetu wakaja kuniomba sana niwaombee wapangwe trafiki. Wamekuja na kazi tofauti. Nikamuuliza kwanza, wewe kwani ni lazima uombe upangwe trafiki?

"Akasema ukienda trafiki acha! Maisha yanakwenda haraka haraka bwana! Unanyanyuka haraka haraka, lakini wa pili nilipomuuliza akaniambia bwana kule kwetu kuna trafiki anaitwa Cheupe.

"Yeye huwa anaongoza misafara ya viongozi. Ana mbwembwe kwelikweli akiwa njiani. Akaniambia mimi namhusudu sana Cheupe, nataka niende trafiki nipewe pikipiki, nifanye kama Cheupe anavyofanya. Kwa namna moja, Cheupe amewa-'inspire' watu waingie trafiki, lakini huyu mwingine akasema bwana, hata nikikosa trafiki nipangwe bandarini. Sasa IGP, hebu rekebisha hili," alisema.

**BODABODA NI SHIDA**

Kuhusu ajali zinazosababishwa na waendesha pikipiki maarufu bodaboda, Rais Samia, alisema takwimu zinaonyesha kuwa waendesha pikipiki hao, bado ni miongoni mwa kundi kubwa linalosababisha ajali.

Alisema ukiangalia takwimu zilizosomwa, utaona kwa kipindi cha miaka mitatu, jumla ya wapanda pikipiki 2,220 wamepoteza maisha kutokana na ajali za barabarani na majeruhi ni 4,202.

"Hii ni sawa na kusema kwa mwaka mmoja, tumepoteza vijana 445 kwa mwaka wanaoendesha bodaboda peke yao; na hospitali zetu zinao vijana 850 kila mwaka," alisema.

**AKATAA MATUMIZI YA FAINI**

Katika hotuba yake, Rais Samia, alisema haungi mkono pendekezo la Baraza la Taifa la Usalama Barabarani, kuomba kutumia nusu ya fedha zinazokusanywa kwenye tozo mbalimbali za ajali au makosa ya barabarani.

"Mmetaka niseme jambo ili mioyo yenu ipone kuhusu fedha kutoka serikalini. Sasa hilo nitalisema baadaye, lakini nikiwa na mapendekezo. Mmekuja na pendekezo kwamba mruhusiwe kutumia nusu ya zile fedha zinazokusanywa kwenye tozo mbalimbali za ajali za barabarani au makosa ya barabarani wazo ambalo mimi binafsi siliungi mkono kwa sababu tozo zile tumeziweka kwamba ni adhabu kwa wakosaji," alisema.

**APACHIKWA 'BI-TOZO'**

Rais samia alisema kila anapokwenda sehemu, amekuwa akiitwa 'Bi- Tozo' lakini kwa nia nzuri ya maendeleo ya taifa na zitaendelea kuwapo ili kuleta maendeleo ya kweli katika sekta mbalimbali.

Awali, IGP Sirro, alimshukuru Rais Samia, kwa uwezeshaji alioufanya Septemba na Oktoba, mwaka huu, kwa kulipa madeni ya watumishi yanayofikia Sh. bilioni 16.1

Kwa mujibu wa Sirro, madeni ya wazabuni yalikuwa Sh. bilioni 8.4, watoa huduma Sh. milioni 815 na madeni ya watoa huduma kwa mwaka 2018 na 2019 yalikuwa Sh. bilioni 19.9

***Imeandikwa na Cynthia Mwilolezi na Godfrey Mushi***


IN THE DISTRICT COURT OF KINONDONI
AT KINONDONI

CIVIL CASE NO 62 OF 2021
AUA INDUSTRIAL GROUP LIMITED..............................PLAINTIFF
*VERSUS*
EMEC ENGEINEERING LIMITED.................................. DEFENDANT

TO:
EMEC ENGEINEERING LIMITED

NOTICE OF DATE JUDGEMENT

**THE NOTICE** that the above case has been fixed for Judgement on 26TH day of NOVEMBER 2021 .at ~~8.30 a.m.~~ 1.00pm

Before **HON.JACOB-RM**

**YOU ARE** required appearing in this Court without fail and you must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of you case.

Given under my Hand and the Seal of the Court this 15th day of November 2021

..............................

RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE
KINONDONI DISTRICT COURT
DAR ES SALAAM

DISTRICT MAGISTRATE COURT KINONDONI, DAR ES SALAAM

*COPY TO BE SERVED UPON:*

..................................................
..................................................
..................................................

116584902


# Msuya: Marekebisho ya Katiba hayaepukiki

**Na Thobias Mwanakatwe**

WAZIRI Mkuu mstaafu, Cleopa Msuya, amesema suala la marekebisho ya katiba haliepukiki Tanzania kwani katiba sio jiwe au amri ya Mungu.

Alisema hayo katika mahojiano na Kipindi cha Dakika 45, kinachorushwa na runinga ya ITV kuhusu tathmini ya miaka 60 ya uhuru wa Tanganyika mambo yaliyofanyika kipindi hicho na yaliyofanyika sasa.

"Katiba si kitu ambacho ni kama jiwe au kama amri ya Mungu, katiba ni kitu ambacho kitarekebishwa from time to time kulingana na mazingira yanayojitokeza," alisema.

Msuya alisema kwa msingi huo, marekebisho hayo ya katiba yatategemeana na makubaliano ya vyama au waliopo kwenye madaraka 'how to move' (namna ya kusonga mbele) na katiba iliyotengenezwa au watakuwa na mpangilio mwingine kwa kuondoa vile vitu wanavyoona havifai.

**ASIFU HATUA YA JK**

Alisema Rais wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete, alikwenda vizuri katika suala hili la katiba kwa kuunda Tume ya Jaji Warioba ambayo ilizunguka nchi nzima wakatengeneza mapendekezo na likaundwa Bunge Maalum la Katiba ambalo lilipendekeza Katiba Pendekezwa ambapo ilibaki stage (hatua) moja tu ya kuipitishwa na wananchi kwa kura ya maoni.

**VYAMA VYA SIASA**

Akizungumzia kuhusu demokrasia katika mfumo wa vyama vingi kwa siasa, Msuya alisema inashangaza kuona Tanzania kuna utitiri wa vyama kati ya 19 hadi 22 vilivyosajiliwa katika Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini.

"Sasa unajiuliza Tanzania hii demokrasia tunaiyotafuta kwenye vyama 22 ni nini hasa, wakati bado tuna sehemu ambazo watu wana njaa, bado tuna sehemu ambazo wabunge wanaomba barabara zijengwe, hivi kweli seriously unasema tuna haja ya vyama vingi?" Alihoji.

Msuya alisema demokrasia anayoiona isiwe na utititri wa vyama vingi vya siasa bali kutafutwe njia ya kuwa na vyama vichache kama vitatu au vinne na isiwe kulazimisha bali wananchi waulizwe kwa kupiga kura na mwisho wa matokeo ya kura utakuta kuna vyama ambavyo hawavitaki.

"Kuna vyama katika hivi 22 kwenye uchaguzi havikupata hata kura 1,000, nchi nyingine wanachokifanya ni kuwa vile ambavyo havikufikia kiwango fulani wanavifuta na kubakia vile ambavyo kiasi fulani vinakubalika," alisema, ambaye alikuwa waziri mkuu katika uongozi wa Mwalimu Julius Nyerere na Ali Hassan Mwinyi.

Msuya alisema kimsingi si vizuri kuwa na chama kimoja tu cha siasa, maana watu wakikaa na chama kimoja wanaweza wakajisahau, hivyo kunahitajika watu ambao wanapiga kelele wanapoona watawala au chama wanaficha madhambi yanayotendeka katika system (mfumo).

"Mimi nakubali mfumo wa vyama vingi uendelee kuwapo, lakini vyama visiwe vingi kiasi hicho, na sasa hivi mtu akishaitwa mwanasiasa anazungumza hata mambo ya uongo, lakini lile lengo la kusaidia serikali inayokuwapo madarakani halipo, wanataka tu wao waingie," alisema.

Aliongeza kuwa kule ambako tumefungua milango kwenye utitiri wa vyama na utitiri wa wanasiasa imekuwa ni shida, inahitaji kuwa na vyama vichache kwani si wengi wanaoelewa dhana ya kuwa na vyama vingi na wanaweza kuwa serikali mbadala kwa kuchunguza makosa ambayo yanafanywa na serikali iliyopo.

Msuya alisema mataifa kama Ujerumani, Korea Kusini, Japan, Malaysia na Singapore yameweza kupiga hatua haraka kimaendeleo kutokana na ushirikishaji wa wananchi katika maendeleo, lakini si kwa kuwa na utitiri wa vyama.

Aidha, alisema Tanzania ina uhuru sana wa watu kujieleza, lakini shida iliyopo ni baadhi ya watu wenye kutoa manung'uniko kuvuka mipaka na hata baadhi ya watumishi wa serikali wa vyombo vya dola kuna wakati wanazidisha udhibiti wa hali hiyo.

## HABARI KITAIFA

### KESI YA SABAYA

# Shahidi adai alitishiwa maisha asipotoa mil. 90/-

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MFANYABIASHARA Francis Mroso (44), amedai mahakamani kuwa aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, alimtishia atampoteza endapo atashindwa kumpatia kiasi cha Sh. milioni 90 ambazo alizihitaji kutoka kwake.

Mroso, ambaye ni shahidi wa 10 katika kesi ya uhujumu uchumi, alitoa madai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, Patricia Kisinda.

Alidai kuwa Sabaya alimwambia asipotoa fedha hizo, watampoteza na kumsababishia kuingiwa na hofu ya kupotezwa na kufunguliwa kesi ya uhujumu uchumi ambayo haina na dhamana.

Washtakiwa wengine, katika shauri hilo ni Silvester Nyengu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31).

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Tersila Gervas, alidai ushahidi pekee unaoweza kuithibitishia mahakama kwamba Januari 22, mwaka huu, alitoa fedha katika Benki ya CRDB tawi la kwa Murombo Sh. milioni 90 ni video ambazo zilizorekodiwa na CCTV camera na Bank Statement.

Kadhalika, alidai kwamba CCTV camera ilirekodi tukio zima ikionyesha akishuka kwenye gari lake kuingia benki huku akiwa ameambatana na vijana wawili wa Ole Sabaya.

Alidai, akionyeshwa video zilizorekodiwa kwenye CCTV camera hiyo, ataitambua kwa kuwa matukio yote, yatakuwa yamerekodiwa wakati akikabidhiwa Sh. milioni 90 zilizokuwa zimewekwa.

Pia, alidai Januari 23, mwaka huu, yalirekodiwa magari matatu kwenye kitabu cha kuhifadhi kumbukumbu ya magari yaliyoingia na kutoka katika gereji yake (karakana).

Alidai alionyeshwa mahakamani kitabu cha kuhifadhia kumbukumbu ya magari yaliyoingia na kutoka karakana hiyo yenye usajili wa namba T144 TZU, STL 5434 na T846 CTU na baada ya kuhakiki alitiki namba hizo.

Mroso, alidai kwamba mzee Marandu ambaye ni mlinzi katika karakana hiyo, alimuuliza kwanini alikwenda kuhakiki namba za magari hayo, na alimweleza kwamba Sabaya, alimlazimisha kutoa Sh. milioni 90, ili asimfungulie kesi ya uhujumu uchumi.

"Baada ya siku tano nilikwenda kwa aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Kenani Kihongosi, kumwomba ushauri namna atakavyonisaidia baada ya kuporwa na kunyang'anywa fedha hizo, na aliniambia nimpatie uthibitisho wa kuonyesha kwamba nilitoa fedha na nilimpatia karatasi ya benki niliyoitumia kutoa hela," alidai shahidi huyo.

Alidai kwamba Mkuu huyo wa wilaya, alitoa kopi ya nyaraka hiyo ya benki aliyotolea fedha hizo huku karatasi halisi (original) na alimwagiza kuhifadhi, na suala hilo atalifikisha katika mamlaka ya juu ya uteuzi kwa kuwa haiwezekani mtu kutoka wilaya nyingine, kwenda Arusha kuchukua fedha bila ya kufuata utaratibu.

Alidai kwamba alipotoka kwa Mkuu wa wilaya, baada ya siku kadhaa alipigiwa simu na mtu wa aliyejitambulisha kwamba ni ofisa kutoka Usalama wa Taifa, akimuuliza kama aliripoti suala la kunyanganywa fedha na Sabaya kwa kiongozi huyo wa wilaya na alithibitisha kwamba ni kweli na ofisa huyo alimweleza kwamba angempigia simu wakati mwingine ili wakutane kwa ajili ya mazungumzo.

Shahidi huyo aliendela kudai mahakamani kwamba baada ya kutoka kwa kiongozi wa wilaya siku zilikwenda hakupigiwa simu tena, lakini Februari mwaka huu, alichukua jukumu la kwenda kwa aliyekuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha (RPC), Salumu Hamduni kumweleza tukio la kulazimishwa kutoa fedha hizo.

Alidai baada ya kutoa ripoti hiyo, siku moja wakati anaendelea na shughuli zake, akiwa eneo la kwa Iddi Ngaramtoni, walifika vijana wawili wakamgongea kioo akiwa ndani ya gari ili afungue na aliwatambua vijana hao kuwa ni wa Sabaya kwa kuwa walikuwapo wakati anatoa fedha hizo.

"Nilishuka kwenye gari kijana mmoja aliniambia kwamba Sabaya ananiita na niliongozana nao kumfuata na nilimkuta ameka kwenye kiti akiwa na vijana wake wengine na tulisalimiana naye.

"Baada ya kusalimiana naye aliniambia kwamba amesikia kwamba mimi ninamtafuta na nilimjibu hapana sijamtafuta, aliniambia mbona nilikwenda kumshtaki kwa DC, nilimweleza nimekwenda kutafuta mwongozo wa kupata fedha zangu na aliniambia kwamba ninadhani kuwa huyo niliyekwenda kushtaki kwake atamfanya nini.

"Sabaya aliniambia hivi, nikisikia Rais amemteua kuwa RC wa mkoa nitafanyaje, nilimwambia alichukua hela zangu nyingi, na pia alisema hizo fedha ni za kwao sisi tumewahifadhia tu, huku akidai kwamba kuwa yeye na vijana walipanga kwenda tena kuchukua kiasi kingine cha fedha Sh. milioni 10," alidai.

Alidai kwamba alimwomba kumrudishia hata kiasi kidogo cha fedha, lakini alimjibu kuwa kama alikuwa anataka iwe hivyo angelimfuata ofisini kwake na siyo kwenda kushtaki kwa DC wa Arusha.

Alidai kwamba Februari mwaka huu, alipigiwa simu na Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoa wa Arusha (RCO), akimtaka kufika ofisini kwao, kwa kuwa alipokea taarifa kutoka kwa RPC kuhusu tukio la kuchukuliwa fedha.

Alidai baada ya mahojiano kumalizika alipigiwa simu kufika katika ofisi za Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mkoa wa Arusha, wakitaka kupewa ripoti kamili ya kuporwa fedha na aliwaeleza tukio lilivyokuwa na baada ya kumaliza kumhoji walimwambia kwamba watafika ofisini kwake kwa kuwa kuna nyaraka wanazihitaji.

Pia alidai Mei 13, mwaka huu, maofisa hao, walikwenda katika eneo hilo, wakihitaji baadhi ya nyaraka ikiwamo karatasi aliyoitumia kutoa fedha benki, kitabu ambacho walikitumia kuhifadhi kumbukumbu cha kurekodi magari yanayoingia na kutoa, leseni yake ya biashara, TIN ya biashara na cheti cha usajili wa biashara.

Pia shahidi huyo, aliwatambua mahakamani washtakiwa hao, akiwamo Sabaya kuwa alitaka ampatie Sh. milioni 90, Watson Mwahomange, Enock Togolani, Jackson Macha, Nathan Msuya (aliwatambua washtakiwa wote kasoro Silvester Nyegu).

Akijibu hoja hizo, Wakili Mwandamizi, wa Serikali, Othmed Mtenga, alidai kwamba shahidi huyo aliomba kutoa nyaraka hizo, kwa kuwa anazifahamu na zimewasilishwa mahakamani kwa mujibu wa sheria.

Hakimu Kisinda, aliahirisha kesi hiyo hadi leo atakapotoa uamuzi mdogo wa pingamizi.

# Tanzania yapokea dozi 499,450 chanjo ya corona

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imepokea chanjo 499,590 ya UVIKO-19 aina ya Pfizer-Biontech kupitia mpango wa COVAX Facility kutoka Marekani ambazo zitakinga Watanzania 249,795 watakaopatiwa dozi hiyo mara mbili.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akipokea chanjo hizo katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA).

"Hadi sasa tumeshapokea jumla ya dozi 1,227,400 za Jensen ambazo zinakinga Watanzania 1,227,400 (dozi moja) na dozi 2,578,400 za Sinopharm ambazo zinakinga Watanzania 1,289,200 (kwa dozi mbili) na leo (jana) tumepokea dozi 499,590 za Pfizer," alisema.

Alisema hadi kufikia Novemba 19, takwimu zinaonyesha waliopata chanjo ni wananchi 1,359,624.

Alisema kati yao wananchi 988,293 (1.7%) ya Watanzania wamemaliza chanjo na kupata kinga kamili dhidi ya ugonjwa huo kwa kuchanja dozi moja ya Jensen na wengine dozi mbili ya Sinopharm.

Alisema wananchi 371,331 (0.6%) ya Watanzania wamechanja dozi moja ya Sinopharm.

"Ninawapongeza wananchi waliojitokeza kupata huduma hii na kukamilisha chanjo, wamechukua uamuzi sahihi wa kulinda afya zao na wananchi wengine hususani kwa mikoa 10 inayoongoza sasa ambayo ni Dar es Salaam, Kilimanjaro, Dodoma, Arusha, Mwanza, Ruvuma, Mbeya, Morogoro, Mtwara na Kagera," alisema.

Waziri Gwajima aliwataka ambao hawajapata chanjo, wafanye haraka kuipata na kusisitiza kuwa UVIKO-19 bado upo na waendelea kuwapoteza ndugu.

"Ninampongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kujali taifa hili na kutuletea huduma hii ya chanjo, dozi hii itawapatia wananchi fursa ya kuchagua chanjo wanayotaka, chanjo hii kama ilivyo ya Jensen na Sinopharm zimethibitishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) kuwa ni bora," alisema.

Alisema wizara yake itafanya wajibu wake wa kujiridhisha na uhakiki wa ubora wa chanjo hiyo kupitia wataalamu na mamlaka husika kabla ya kuanza kutolewa kwa Watanzania.

MIAKA 60 YA UHURU

Ofa Maalum
KIFURUSHI CHA UHURU




IPP MEDIA INATOA OFA YA PUNGUZO LA BEI KWA MATANGAZO YATAKAYOWEKWA KATI YA NOVEMBA 15 HADI DESEMBA 15, 2021 KWA MATANGAZO YA MIAKA 60 YA UHURU

KWA MAULIZO YOTE WASILIANA
SIMU NA. 0713 217955, 0782253676 AU 0787633313

The Guardian | Nipashe | ITV | EATV | eastafrica RADIO

HABARI KITAIFA

# Shahidi abanwa na kukiri ushahidi wake kutokuwamo kwenye maelezo

**Na Kulwa Mzee**

SHAHIDI wa tatu katika kesi ndogo, Sajini Goodluck, kwenye kesi ya ugaidi inayomkabili mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na wenzake watatu, amebanwa maswali na kukiri kwamba sehemu ya ushahidi anaotoa mahakamani haupo kwenye maelezo yake aliyotoa Desemba 10, 2020.

Akihojiwa na Wakili wa Utetezi, Jeremiah Mtobesya kutokana na ushahidi wake, alidai alipotoka na watuhumiwa, Adamu Kasekwa na Mohammed Ling'wenya mjini Moshi, aliungana na Afande Swila, Dar es Salaam.

Alidai kuwa hafahamu Afande Swila yuko kituo gani lakini anakumbuka aliandika maelezo yake Desemba 10, 2020, kuelezea alifanya nini katika tukio lote la kuwakamata watuhumiwa Rau Madukani Agosti 5, 2020 hadi kuwafikisha Dar es Salaam Agosti 7, 2020.

Alipotakiwa kueleza mahali gani aliandika, alidai kuwa alizunguka na watuhumiwa baada ya kuwakamata wakimtafuta mtuhumiwa mwenzao, Moses Lijenje. Akijibu swali hilo, alidai hakuna mahali popote katika maelezo yake aliandika hayo na hakuna mahali aliandika baada ya kuwafikisha Kituo cha Polisi Kikuu cha Moshi watuhumiwa pamoja naye hawakushuka kwenye gari. Shahidi alikiri kwamba hakuna mahali katika maelezo yake alipoandika kwamba baada ya kumtafuta Lijenje bila mafanikio aliwarudisha watuhumiwa kituoni Moshi saa 5:00 usiku na kuwakabidhi.

Baada ya kudai hayo, Wakili Mtobesya aliomba maelezo ya shahidi huyo yapokewe kama kielelezo cha upande wa utetezi, mawakili wa Jamhuri hawakupinga na kielelezo hicho kilipokewa.

Akihojiwa na Wakili John Mallya, shahidi huyo alidai wakati wanakwenda kuwakamata watuhumiwa, alibeba silaha, lakini katika ushahidi wake hakuna mahali alipoeleza kwamba kuna wakati aliiacha mahali.

Shahidi alidai kuanzia Agosti 5 hadi 7, 2020, alikuwa anaimarisha ulinzi kwa watuhumiwa lakini katika maelezo yake hakuna mahali alipoandika kwamba alikuwa na jukumu hilo.

Pia katika maelezo yake, hakuandika kwamba wakati wanakwenda kuwakamata watuhumiwa walikuwa askari watano.

Katika ushahidi wake wa awali, akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Pius Hillar, Sajini Goodluck alidai si kweli kwamba Ling'wenya aliteswa na kulazimishwa kutia saini maelezo kwenye karatasi.

Alidai si kweli kwamba watuhumiwa hawajawahi kufikishwa Kituo Kikuu cha Polisi Dar es Salaam na alidai walifikishwa Agosti 7, 2020 na Agosti 8, mwaka huo, alishiriki kuwahamishia Kituo cha Polisi cha Mbweni.

"Hakuna sehemu yoyote ambapo watuhumiwa waliteswa, sikuwatesa sababu baada ya kuwafikisha Mbweni tuliondoka," alidai Goodluck. Alidai Agosti 9, 2020 akiwa na Inspekta Mahita Omary walikwenda kumkamata Halfani Bwire na kumpeleka Kituo cha Polisi Chang'ombe kisha kwenda kufanya upekuzi nyumbani kwake Temeke na kukuta vifaa mbalimbali vya jeshi katika mfuko unaoitwa shangazi kaja.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Bwire, Mbowe, Kasekwa na Ling'wenya ambao wanakabiliwa na mashtaka sita ikiwamo kula njama kufanya vitendo vya kigaidi.




Mwenyekiti wa Taasisi isiyo ya kiserikali ya Volunteers in Development (VID), Time Shaaban, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu matembezi ya hisani ya kuchangisha pesa za kusaidia watoto zaidi ya 800, wanaoishi katika vituo mbalimbali vya kulelea watoto hao hapa nchini. Kulia ni Katibu Msaidizi wa Taasisi hiyo, Shadya Awadh. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# THBUB yatoa neno usalama barabarani

**Na Christina Mwakngale**

TUME ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), imesema serikali iendelee kuboresha miundombinu ya barabara na kusimamia sheria za usalama barabarani na kuhimiza matumizi ya teknolojia saidizi, kuwezesha ukaguzi wa magari kwa ufanisi na uwazi.

Kadhalika, imesema vituo vya ukaguzi na vifaa vya kisasa kwa askari wa usalama barabarani, vifaa vya kisasa vitaongeza ufanisi na kwamba matakwa ya sheria inayomtaka kila mwajiri kutoa mikataba ya ajira kwa madereva isimamiwe.

Makamu Mwenyekiti wa THBUB, Mohamed Khamis Hamad, aliyasema hayo jana katika taarifa yake, ikiwa ni kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani yenye kauli mbiu 'Jali Maisha yako na ya Wengine Barabarani'.

Alisema Jeshi la Polisi na wadau wengine waendelee kutoa elimu kwa madereva na wananchi kuhusu matumizi sahihi ya barabara ili kuepusha ajali na kuhimizwa kuzingatia sheria za usalama barabarani.

"Usimamizi duni wa kisheria kwa baadhi ya maeneo, husussan magari ya abiria safari ndefu kuwa na dereva mmoja, kutokuwa na mikataba ya ajira, upotevu wa haki za waathirika wa ajali; kunaweza kuongeza vifo vitokanavyo na ajali.

"Tunatoa pongezi kwa serikali kwa hatua mbalimbali zilizochukuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa na vyombo vyote vinavyohusika na usimamizi wa sheria za usalama barabarani," alisema Hamad.

Aidha, tume hiyo ilisema, kuboreshwa kwa miundombinu ya barabara, imesaidia kupungua kwa vifo na majeruhi kutokana na ajali za barabarani.

# Chongolo amtaka Mbarawa kupeleka barabara Tabora

**Na Beatrice Shayo,** TABORA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amemtaka Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa, kutekeleza ilani ya uchaguzi ya chama kwa kuwa ni wajibu wake kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara.

Chongolo alitoa kauli hiyo jana baada ya kupata malalamiko kutoka kwa Mbunge wa Manonga, Seif Gulamali, wakati wa ziara ya kiongozi huyo akiwa kata ya Simbo Wilaya ya Igunga mkoani Tabora alipofika kukagua utekelezaji wa ilani na kuhimiza uhai wa chama ngazi za mashina.

Gulamali alilaumu serikali kutojenga barabara ya Ndala-Simbo-Nkinga-Ziba mpaka Shinyanga Vijijini kwa muda mrefu huku waziri akiwaambia atafikiria endapo hiyo barabara itajengwa.

Chongolo alisema waziri huyo hatakiwi kufikiria kujenda na kwamba ni wajibu wake kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo na kutekeleza Ilani ya Chama.

"Hatutaki Waziri afirikirie. Ni wajibu wake kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi na utekelezaji wa Ilani. Waziri anayefikiria kutimiza wajibu wake hana uhakika," alisema. Pia alisema waziri anatakiwa kuwajibika kutimiza wajibu wake kwa sababu chama kilishaahidi mwaka 2020 na ndani ya miaka mitano ni lazima kitekeleze.

Kiongozi huyo aliwaeleza wananchi kuwa akirudi ofisini kwake atamtaka Waziri ampe mpango wa utekelezaji wa barabara hiyo ili iweze kujengwa kwa kuanzia mwaka ujao wa fedha wa 2022/23.

Aidha, Chongolo alisema mawaziri wote wanatakiwa kutekeleza ilani bila kufikiria ili kutatua changamoto zinazowakabili wananchi.

"Nimeona umeme hapa, nitarudi na kumuuliza Waziri wa Nishati mpango wa kuhakikisha Desemba mwakani vijiji vyote vya jimbo la Manonga na Tabora vinapata umeme na umefikia wapi kwa sababu hiyo ndiyo ahadi ya CCM na inatakiwa itekelezwe na serikali," alisema Chongolo.

Alisema CCM ikiacha mawaziri wafanye kwa kufikiria, watavuka kipindi hicho umeme haujafika na wao waliahidi wamekabidhi jukumu la kutenda walichoahidi kwa serikali ni lazima wasimamie utekelezaji wake.

"Sisi tulichoahidi hatuko tayari kuwa waongo ni lazima tushikane mashati kutimiza kile ambacho tuliahidi na hiyo ni kazi ya CCM na Mwenyekiti wa CCM na Rais Samia Suluhu Hassan amenituma kufanya haya"alisema.

HABARI KITAIFA

# Mawakili Tanzania wang'ara tuzo elimu unyanyasaji kingono

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Wanasheria wa Kimataifa (IBA), kimezitangaza Kampuni za Uwakili za Baker McKenzie, Clifford Chance, IMMMA Advocates na DLA Piper kuwa washindi wa 2021 wa Tuzo za Wanachama wa IBA kwa Ulaya na Afrika.

Tuzo hizo zilizotolewa Novemba 18, mwaka huu kwa kutambua usaidizi wa kipekee wa kampuni hizo kisheria na michango katika kazi, miradi, malengo muhimu na matarajio ya IBA. Rais wa IBA Sternford Moyo, Mwenyekiti na Mshirika Mwandamizi wa kampuni ya wanasheria ya Scanlen and Holderness ya nchini Zimbabwe, alisema uungwaji mkono, kujitolea na kutunukiwa tuzo na IBA husaidia kuchagiza mustakabali wa taaluma ya sheria duniani kote.

"Kila kampuni ni mfano mzuri wa jinsi wataalamu wa sheria waliojitolea wanavyotumia vyema taaluma yetu na hivyo basi kuisaidia jamii kwa ujumla kwa sababu sheria inagusa kila nyanja ya maisha. Usaidizi wao thabiti huongeza ufikiaji wa malengo ya IBA," alisema Moyo.

"Tunayo furaha kutambua mafanikio ya kampuni hizi za sheria za kimataifa kwa tuzo zetu za Wanachama wa Kikundi za 2021," aliongeza.

Mkurugenzi Mtendaji wa IBA, Dk Mark Ellis, alisema njia za kimantiki ambazo kundi la washindi wa tuzo za 2021 za wanachama wa IBA huleta mabadiliko chanya kupitia mazungumzo, utekelezaji wa sera mpya na ushirikiano wa kutiana moyo. Alisema kujitolea kwa kampuni hizo na kuunga mkono, kazi ya IBA inahimiza miradi na vitendo vya ujasiri miongoni mwa wanachama.

Akisoma tuzo hizo alisema, Tuzo za Mwanachama wa Kundi la Ulaya na Afrika 2021 IBA zilienda kwa Baker McKenzie kwa kampeni yake kubwa na nzuri ya kukuza IBA, ambayo iliangazia kazi za chama kuendeleza utawala wa sheria na kushughulikia masuala ya upatikanaji wa haki.

Kampeni hiyo iliwahimiza wanasheria wake kujihusisha na IBA. Hatua hiyo ilielezwa kusababisha mawakili 4,580 wa Baker McKenzie kuletwa katika kundi la IBA ambao ni pamoja na Wakili Poulton, Mshirika Msimamizi katika Baker McKenzie London ambaye alisema tuzo hiyo imewapa ari mawakili wengi zaidi kujiunga na IBA.

"Ninajivunia sana kukubali Tuzo hii ya Mwanachama wa Kundi kwa niaba ya Kampuni ya Baker McKenzie kwa kazi yetu ya kuunga mkono Chama cha Wanasheria wa Kimataifa. Hii imesababisha zaidi ya watu wetu 4,500 kujihusisha na IBA," alisema Wakili Poulton.

Kampuni za IMMMA Advocates na DLA Piper zilipewa tuzo kwa kushirikiana kupitia kuunga mkono na kudhamini kazi za IBA barani Afrika zilizohusiana na kutoa elimu ya madhara ya unyanyasaji wa kingono na rushwa na hivyo kuongeza uelewa kwa wananchi barani Afrika.

Akitoa maoni yake baada ya kupewa tuzo hiyo, Sadock Dotto Magai, Mshirika Msimamizi katika Kampuni ya Uwakili ya IMMMA kutoka Tanzania, alisema ushiriki wao katika kazi za IBA ulisaidia kuongeza uelewa kuhusu athari za unyanyasaji wa kingono na rushwa.

"Kuhusika kwetu katika mradi kulifungua macho yetu na wengine katika kujenga ufahamu wa kuelewa hatari ya ngono kama uhalifu, rushwa na unyanyasaji wa kingono kwa watu walio katika mazingira magumu, tutaendelea kuwa mabalozi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kukuza uelewa wa athari ya ngono," alisema Magai.

## Mabula awashukia watendaji wakaidi

**Na Munir Shemweta,** BUKOBA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameanza kuchukua hatua kwa watendaji wa sekta ya ardhi wanaoshindwa kutekeleza maagizo anayoyatoa wakati wa ziara zake.

Katika kuchukua hatua hizo, amemtaka Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Kagera, Erick Makundi, kuwaandikia barua za kujieleza watumishi wawili wa Halmashauri na Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera.

Watumishi wanaotakiwa kujieleza kwa nini wasiondolewe katika nafasi zao ni Mkuu wa Idara ya Ardhi na Mipango Miji, Catres Rwegasira na Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili ambaye pia ni Ofisa Ardhi Mteule wa Halmashauri hiyo, Fidelis Alute.

Hatua ya Naibu Waziri Mabula inatokana na watendaji hao kushindwa kutekeleza maagizo waliyopewa kwa nyakati tofauti na Naibu Waziri huyo akiwa katika ziara zake mkoani Kagera kwa ajili ya ufuatiliaji wa utendaji kazi wa sekta ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri, kokote atakapopita na kukuta hakuna utekelezaji wa maagizo aliyoyaacha, atachukua hatua kali kwa wahusika lengo likiwa ni kujenga nidhamu na kuhakikisha kero za wananchi katika masuala ya ardhi zinashughulikiwa.

Dk. Mabula ambaye alikuwa akizungumza na watendaji wa sekta ya ardhi katika Manispaa na Halmashauri za Bukoba mkoani Kagera juzi, alisema kutokana na baadhi ya watumishi wa ardhi kufanya kazi kwa mazoea, kuna haja ya kuwabadilisha vituo vya kazi hasa waliokaa muda mrefu kwenye kituo kimoja.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA KWA AJILI YA KUTOA HUDUMA YA MALIPO YA MSHAHARA KATIKA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (EACOP) NCHINI TANZANIA – KUMBUKUMBU NA. 0010007291**

TotalEnergies East Africa Midstream B.V (Kampuni) Tanzania, Kampuni ya Mafuta na Gesi, itahitaji katika utekelezaji wake huduma ya Mkandarasi mwenye uzoefu na sifa kutoa huduma ya malipo ya mshahara. MKANDARASI atapewa jukumu la, lakini lisilojikita tu kwenye, kukusanya taarifa, maandalizi ya orodha ya wanaotakiwa kulipwa mshahara, kufanya mahesabu ya mshahara, kutoa risiti za malipo na kufanikisha shughuli zote za baada ya kufanya malipo.

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba lililofukiwa chini la kusafirisha Mafuta linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Mkoa wa Tanga, Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania na kilomita 296 zitakuwa nchini Uganda.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**

Mradi wa EACOP unajiandaa kuajiri katika nafasi mbalimbali kwenye Kampuni na linahitaji usaidizi wa shughuli za Usimamizi wa Rasilimali watu kwa waajiriwa hawa.

EACOP inahitaji huduma ya malipo ya mshahara kutoka kwa mtoa huduma atakayetoa usaidizi katika kampuni kwa ajili ya kusimamia ulipaji wa malipo na matakwa ya kodi. Mhudumu atakayechukuliwa ataandaa orodha ya malipo kwa kila mwezi, atakusanya taarifa, maandalizi ya orodha ya wanaotakiwa kulipwa mshahara, kufanya mahesabu ya mshahara, kutoa risiti za malipo kwa kuzingatia usiri na kufanikisha shughuli zote zinazofuata baada ya kufanya malipo.

Mtoa huduma atakayechaguliwa atachakata taarifa za kodi na kodi za mwisho wa mwaka. Vilevile, mtoa huduma atakayetakiwa anatakiwa kuwa na uzoefu kwenye: miundombinu ya kieletroniki ya kulipa mshahara, mfumo wa kodi wa Tanzania, aweze kuzingatia sheria za nchi, viwango vya utendaji vya Kimataifa, na sheria ya ajira ya nchini Tanzania.

Mawanda yatahitaji wakandarasi kuwa na uelewa wa Mafuta na Gesi, uelewa wa kampuni ya EACOP na Mradi.

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni/Mashirika yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uzoefu usiopungua miaka 10 katika kutekeleza majukumu tajwa kwa uwanda mpana nchini Tanzania, kwa kuzingatia viwango vya kitaifa na Kimataifa.
- Idadi ya wataalam wenye vigezo na uzoefu katika maeneo tajwa.
- Uwezo wa kifedha kwa ajili ya kutekeleza mkataba.
- Uzoefu wa kuetekeleza sera husika za Ubora wa Afya, Usalama na Mazingira, utaratibu na mchakato kwa ajili ya uzabuni kwa kuzingatia viwango vya tasnia husika na vya nchi.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani na sheria za Kitaifa na Kimataifa pamoja na viwango vya Kimataifa vya mafuta na gesi.
- Uthibitisho wa sera ya mkandarasi ya Ubora wa Afya, utaratibu na mchakato kwa kuzingatia viwango vya nchi na tasnia husika kwa kazi zinazohusiana.
- Usajili stahiki kutoka kwa mamlaka husika ndani ya nchi kwa ajili ya kutoa huduma tajwa.
- Uthibitisho wa usajili katika Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) na Cheti cha Ithibati ya Malipo ya Kodi cha mwaka wa hivi karibuni.

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa **9:00** mchana Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **7 Disemba 2021.** Kichwa cha Barua Pepe ni **0010007291**

**Muhimu:** Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA).

21658170

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Siku 16 Kupinga Ukatili zituvushe hatua kubwa

**MAADHIMISHO** ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia dhidi ya wanawake na watoto zinaanza Novemba 25 hadi Desemba 10, huku maadhimisho yakiongozwa Kituo cha Kimaraifa cha wanawake.

Zaidi ya asasi 6,000 na zaidi ya nchi 187 hushiriki maadhimisho haya ambayo chimbuko lake kupinga unyanyasaji wa kijinsia na mauaji ya kinyama ya kina dada wa Mirabelle yaliyofanyika nchini Dominica mwaka 1990 na mwaka 1991 Umoja wa Mataifa (UN) ulichagua Novemba 25 iwe siku ya kimataifa ya kupinga ukatili wa kijinsia.

Lengo la maadhimisho ni kutoa fursa kwa wanawake, wanaume, vijana wa kike na kiume na wanaharakati wengine kukuza uelewa wa umma juu ya mchango wa wanawake katika maendeleo na kutafakari matokeo ya harakati za ukombozi wa wanawake kimapinduzi pamoja na kutafakari mafanikio hayo.

Tanzania inatajwa kufanya vizuri kwa sasa kuanzia kwenye idadi ya wanawake wanaoteuliwa kwenye nafasi za maamuzi imeongezeka ikiwamo jitihada za wazi kupambana na ukatili wa kijinsia kwa kuwa na madawati ya jinsia kwenye vituo vya polisi.

Rais Samia Suluhu Hassan, anakuwa rais wa kwanza mwanamke kuongoza Tanzania, lakini amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha wanawake na watoto wanainuka kutoka hatua waliyokuwa wameachwa kwenda nyingine.

Juzi nchi za Ulaya, kupitia mabalozi wake nchini kwa kushirikiana na mashirika ya Umoja wa Mataifa ya UN-Women na UNFPA, wakiahidi kuwa mstari wa mbele kupinga ukatili wa kijinsia na ikiwamo kusaidia utekelezaji wa miradi ya kijamii.

Pia NGO za nchini zinashiriki kikamilifu kuadhimisha siku hizi, huku wakipaza sauti ya mabadiliko ya sera, sheria na kanuni ili kusaidia ustawi wa kijamii.

Tunapoazimisha miaka 60 ya Uhuru mengi ya kujivunia ni ongezeko la wanawake wasomi na viongozi waliopo kwenye nafasi za maamuzi, licha vikwazo vinavyosababisha kundi hilo kushindwa kufikia ndoto zake. Bado ukatili huo unaendelea, mfano, Rais wa Zanzibar, Hussein Ali Mwinyi aliamua kuanzisha mahakama ya ukatili wa kijinsia.

Kilio kikubwa cha muda mrefu ambacho kimekuwa kiporo ni Katiba inayomtambua mtu mzima ni kuanzia miaka 18 na Sheria ya Ndoa ya mwaka 1977 inaruhusu mtoto wa miaka 14 kuolewa kwa ridhaa ya wazazi wake.

Hili limetumiwa na baadhi ya jamii kama mbinu ya kujipatia fedha na mali kwa watoto kulazimishwa kuolewa au kufanya vibaya kwenye mitihani yao ya darasa la saba ili wasipate sababu ya kuendelea na masomo, na sasa kuna idadi kubwa ya walioolewa katika umri mdogo.


Ni muhimu tunavyosherehekea miaka 60 ya uhuru serikali kutimiza ahadi yake ya kufanya mabadiliko ya Sheria ya Ndoa, ili kumwepusha mtoto wa kike dhidi ya dhuluma hizo.

Bado kuna ongezeko la ukatili wa kunajisi kwa watoto wadogo na idadi ya watoto wa kiume wanaolawitiwa inaongezeka kila uchao, huku matukio ya ubakaji yakiathiri wengi na kesi nyingi zikiishia kwenye vituo vya polisi na familia.

Tunaona kuwapo nguvu kubwa na kaelekezwa kulinda watoto ambao wanaumizwa kiasi cha kuharibu maisha yao ya baadaye, kwa kuwa tunaamini kila mdau akitimiza wajibu wake tutakuwa na jamii yenye amani na usawa. Lazima kuwe na tofauti ya maadhimisho ya mwaka hadi mwaka, tuone jamii ikipiga hatua kwa kutokuwa na matukio ya ukatili.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

### Mgombea binafsi haki iliyohitaji wa kuitetea

**SAFARI** ya kupigania kuwapo mgombea binafsi au huru kwenye uchaguzi ilianza mwaka 1993, Mchungaji Christopher Mtikila, akiibua ajenda hiyo ambayo hata kwenye katiba ya wananchi ( ya Warioba) ilipendekezwa.

Mtikila aliifungulia kesi ya kikatiba mbele ya Jaji Kahwa Lugakingira, kwenye Mahakama Kuu Kanda ya Dodoma, akitaka haki hiyo.

Jaji Lugakingira, alikubaliana na hoja za mwanasiasa huyo, akisema kusimama kama mgombea binafsi ni haki ya kila Mtanzania kwa mujibu wa katiba.

Aliamini mwenye haki ya kuchagua viongozi ana haki ya kugombea uongozi, lakini baadaye mwaka 1994 serikali ikawasilisha bungeni mapendekezo ya kubadilisha ibara ya 34 ya katiba kwa kuzuia wagombea binafsi.

Mtikila hakuchoka ilipofika 2005 alifungua tena kesi katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam akipinga marekebisho hayo, kesi ambayo ilisikilizwa na majaji watatu.

Ingawa mahakama ilikubali haki ya kila raia kuchagua na kuchaguliwa bila kuwa mwanachama wa chama cha siasa, ilibainisha kuwa si jukumu lake kujielekeza kwenye masuala ya kisiasa.

Mtikila akiwa Mwenyekiti wa DP hakuchoka kupigania mgombea binafsi hadi alipofariki mwaka 2015, na tangu wakati huo, hajajitokeza mwingine kuendeleza ajenda hiyo.

Hivyo, ni suala linalohitaji mtetezi kwani ninaamini kuwa kama ajenda hiyo ingefanikiwa kupenya, ingekuwa ni nafasi ya pekee kwa vijana wanaobanwa na vyama vyao kuwania nafasi za uongozi katika uchaguzi.

Wanufaika wengine wangekuwa ni wale ambao wamekuwa wakikwamishwa kutokana na ukosefu wa fedha au kukataa kutii matakwa ya wakubwa wao ikiwamo kutoa rushwa ya ngono ili wapitishwe.

Ni vyema sasa wale ambao wamekuwa wakikwamishwa na njia hiyo, wakaendeleza pale Mchungaji Mtikila alipoishia katika harakati za kutetea haki ya mgombea binafsi ili kufanikisha demokrasia.

Hatua hiyo ya kuwapo kwa mgombea binafsi pia inaweza kupunguza gharama za kurudia uchaguzi ambazo serikali imekuwa ikiingia pale madiwani au wabunge wanapohama vyama na kusababisha kurudiwa kwa uchaguzi.

Ninaamini kwamba, mfumo wa mgombea binafsi pia unaondoa ukiritimba wa watu kuchaguana kwenye vyama kwa kujuana na kupitishwa bila kupingwa na unaweza kuondoa chuki za kivyama.

Vilevile, mfumo wa mgombea huru unaweza kuwa njia ya kuwapa nafasi vijana wengi kujitokeza kugombea na kuwa viongozi bila vikwazo kutoka kwa wanasiasa wasiotaka kung'atuka.

Hivi karibuni kada wa CCM, Thomas Ngawaiya, analikumbushia suala hilo la mgombea binafsi akidai kuwa mwaka 1960 Tanganyika iliruhusu mfumo huo katika uchaguzi mkuu.

Anafafanua kuwa, TANU ilishinda viti 70 kati ya 71 vya ubunge, huku kimojawapo kikiwa ni cha Jimbo la Mbulu mkoani Arusha ambacho kilichukuliwa na mgombea binafsi Herman Sarwatt, aliyemshinda mteule wa TANU, Chifu Amri Dodo.

Kwenye karne hii ya 21, inawezekana wapo watu wengi ambao si wanasiasa wanaotamani kuongoza, lakini wanakwamishwa na mfumo uliopo wa kupitia kwenye vyama huku wao wakipendelea kuwa wagombea huru.

Mgombea binafsi pia ni njia ya kupanua wigo ili kila Mtanzania mwenye uwezo wa kuongoza apate nafasi ya kuchaguliwa na wapigakura wanaoona kwamba ana uwezo wa kuwaongoza hata kama hana chama.

Pamoja na hayo kuwapo kwa mgombea binafsi pia, kunaweza kuwafanya wabunge au madiwani kuwa na uhuru wa kujieleza wanapokuwa katika vikao au mikutano bila kuogopa ama kuegemea upande wa vyama.

Si vibaya wakajitokeza wanasiasa wengine kubeba bango la ajenda hiyo na kuifanya kazi ili ikiwezekana, Tanzania iige mfano kwa nchi nyingine ambazo zimeruhusu mfumo huo kwa kuangalia faida na hasara zake.

HABARI KITAIFA

## Taasisi yashauri Serikali na vyama vya siasa kukutana

**Na Sabato Kasika**

TAASISI ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), imeshauri kuwapo kwa meza ya mazungumzo kati ya serikali ya vyama vya upinzani ili kuimarisha umoja wa kitaifa.

Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Thomas Ngawaiya, alisema hayo mkoani Dar es Salaam, katika mkutano na waandishi wa habari alipokuwa akizungumzia miaka 60 ya uhuru wa Tanganyika.

"Kumekuwapo na wanasiasa kuwekwa ndani au kufunguliwa kesi, tunaishauri serikali iitishe meza ya mazungumzo kati yake na vyama vya upinzani ili kuwaunganisha kuondoa tofauti hizo," alisema Ngawaiya.

Alisema, maendeleo yanaletwa kwa umoja, na kwamba badala ya kuwekana na ndani, watu wapingane kwa hoja za maendeleo ya taifa lao, kwa madai kwamba wote wanaitakia mema nchi yao.

Alisema watu kuwekwa ndani au kufunguliwa kesi ni jambo la kawaida, bali kuwapo kwa kesi zisizoisha ndiyo tatizo ambazo anaona kuwa kuna haja ya kuwapo kwa meza ya mazungumzo kuangalia namna ya kumaliza tatizo hilo.

Ngawaiya alisema, tangu awamu ya sita imeingia madarakani, baadhi ya watu wametolewa magerezani wakiwamo wanasiasa, kwamba hatua hiyo ni mwanzo mzuri ila kunahitajika kuwapo kwa mazungumzo na wanasiasa.

"Wote wanajenga nyumba moja ambayo ni Tanzania, hivyo ni muhimu kuhakikisha hoja zao zinasikilizwa, ili kasoro zimalizwe kwani siasa ni siasa ni kupingana siyo kupigana na kuwekana ndani," alisema.

Alisema, nchi inapoelekea kwenye maadhimisho ya miaka 60 ya uhuru, CEGODETA inashauri serikali kuendelea kuboresha utawala bora, demokrasia na maendeleo.

"Lakini pia wananchi wote chini ya awamu ya sita, tukelekeze kwa vitendo tunu za taifa ambazo ni amani, umoja na mshikamano pia tuwe na utawala wa kisheria unaozingatia sheria kwa dhati na vitendo," alisema.

# Silaha 24 zasalimishwa kutii agizo la waziri

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani limepokea silaha 24 kutoka kwa raia wa mkoani hapa ambao wametii agizo la Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, alilolitoa Oktoba 30, mwaka huu.

Simbachawene akiwataka wananchi wanaomiliki silaha kinyume cha sheria kuzisalimisha polisi na muda uliopangwa utakapomalizika, utaanza msako wa nyumba kwa nyumba.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema katika siku 22 baada ya kutolewa kwa tamko hilo, silaha aina ya Rifle mbili na risasi 40, bastola moja na risasi saba na magobore 21, ziliwasilishwa katika vituo vya polisi vya Chalinze na Bagamoyo kwa tarehe tofauti.

Kamanda Wankyo aliwataka wananchi wanaomiliki silaha kinyume cha sheria kuendelea kuzisalimisha kutii agizo la waziri katika muda uliotolewa.

Katika tukio lingine, Polisi mkoani Pwani wameendesha oparesheni, misako na doria kwa lengo la kudhibiti makosa ya jinai na katika operesheni hizo, watuhumiwa 21 walikamatwa wakiwamo wanawake watatu na wanaume 18.

Kamanda Wankyo alisema baada ya kukamatwa, watuhumiwa hao walihojiwa na kupekuliwa na kukutwa na televisheni tano, sabufa nne, vitambaa saba, vitenge doti tano na madela manne, vichwa vya cherehani viwili aina ya Singer na Buterfly pamoja na rimoti na deki.

Wankyo alitoi rai kwa wananchi waliovunjiwa na kuibiwa kufika kituo cha polisi Kibaha Mjini kutambua mali zao. Pia aliwataka wananchi kuendelea kutoa ushirikianao kukomesha uhalifu kwenye mkoa huo.



Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo (CEGODETA), Thomas Ngawaiya, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu maendeleo yaliyopatikana nchini katika miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara. Kulia ni Katibu Mkuu wa taasisi hiyo, Hamad Thao. **PICHA: SABATO KASIKA**

## RC ahimiza wataalamu ushirikishaji wananchi katika uhifadhi wa misitu

**Na Christina Haule,** LINDI

WATAALAMU wa misitu wametakiwa kuishirikisha jamii katika usimamizi shirikishi wa misitu (USM) ili kutunza misitu ambayo ni chanzo kikuu cha mvua na kuondokana na mabadiliko ya tabia nchi.

Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainab Telack, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kwamba wataalamu wa misitu hawana budi kuitumia vyema elimu yao waliyopata darasani sambamba na elimu za muda mfupi kupitia mashirika mbalimbali ya uhifadhi wa misitu.

Telack alisema kufanya hivyo kutasaidia kuboresha kilimo ambacho ndicho chanzo kikuu cha uchumi mkoani na nchini kwa ujumla.

Alisema kupitia misitu wanaweza kupata mvua na kuboresha zao la korosho, hivyo kutegemea kuvuna mazao yenye kuleta tija sambamba na kuajiri watu wengine na kupunguza ukosefu wa ajira, tatizo ambalo ni kubwa kwa sasa.

Kuhusu faida za uhifadhi misitu, Telack alisema mwaka 2020 waliuza korosho mkoani hapo na kupata Sh. bilioni 151 na mwaka huu wameshaanza kuuza korosho na kupata Sh. bilioni 71 na kwamba katika ufuta pia wamepata Sh. bilioni 121 kwa mwaka huu.

Alisema bila uhifadhi wa misitu mazao yakiwamo korosho na hayawezi kukua na kuleta tija kwa sababu mazao yoyote yanategemea mvua na kunyesha mvua kunategemea na utunzaji wa msitu uliopo.

Alisema amekuwa akiendelea kuwahamasha wananchi kujituma katika uhifadhi wa misitu na kilimo ili fedha nyingi zinazopatikana kwenye makundi zipatikane pia kwa mtu mmoja mmoja.

"Nimekuwa nikiwaambia natamani kuona fedha kama hizo ziko kwenye mikono ya mtu mmoja, lakini wako wanaopata hadi milioni 80 lakini suala la matumizi kuingizwa katika kuboresha maisha yao bado ni tatizo, hivyo bado wanahitaji elimu," alisema.

Pia aliwataka wakulima mkoani hapa kuacha kukata na kuchoma miti aina ya mipingo wanapoandaa mashamba na kwamba miti hiyo imeanza kutoweka katika maeneo hayo.

Alisema kupotea kwa miti hiyo kutaondoa uasili wa miti iliyopo nchini na kuharibu maana ya uhifadhi wenye faida kutokana na miti aina ya mipingo myeusi kuwa na soko kubwa nje ya nchi lakini pia inaweza kusababisha kutokuwa na vinyago vya kuonyesha uhalisia wa rasilimali za nchi.

Naye Ofisa kutoka Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA), Elida Fundi, alisema kwa sasa wanafundisha wataalamu wa misitu kutoka wilaya ya Kilolo, Liwale na Ruangwa ambako mradi wa kuhifadhi misitu kwa kuwezesha biashara endelevu ya mazao ya misitu Tanzania (CoForEST) upo kwa kuwapa elimu sahihi ya uhifadhi misitu.

Alisema wamekuwa wakiwapa elimu ya namna ya kutenga maeneo, kuyahifadhi na kufanya usimamizi shirikishi wa misitu kwa jamii (USMJ) na wao kusaidia kielimu vijiji vinavyozunguka kijiji husika ili kusaidia misitu isiweze kupotea.

MJUMITA kwa kushirikiana na Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo na ushirikiano la Uswisi (SDC) wanaendesha awamu ya tatu ya mradi huo katika wilaya za Nachingwea, Liwale na Ruangwa mkoani Lindi, Morogoro, Kilosa na Mvomero mkoani Morogoro na Kilolo mkoani Iringa.

# AZAKI: Tanzania ijitathmini utawala bora

**Na Christina Mwakangale**

TANZANIA imeshauriwa kujitathmini kwenye masuala ambayo imefanikiwa, kusifiwa na kuwa mfano wa kuigwa barani Afrika, ili isipoteze sifa hizo kutokana na vikwazo mbalimbali.

Mkurugenzi wa Kituo cha Taarifa kwa Wananchi (TCIB), Deus Kibamba, aliyasema hayo jana kwenye mkutano uliohusisha Asasi za Kiraia (AZAKI), kuangalia nafasi za asasi hizo katika Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Afrika (APRM).

Alisema Tanzania kwenye taarifa ya Tathmini ya Masuala ya Utawala bora (Country Review Report)iliyotolewa mwaka 2013, ilibainika kufanya vizuri kwenye masuala kadhaa, ikiwamo kuanzisha mchakato wa katiba mpya, mwafaka wa kisiasa Zanzibar pamoja na ibara zinazozungumzia ukomo wa kiti cha urais.

"Tanzania tulitajwa tunafanya vizuri, lakini tunakaribia kuyumba. Tanzania inapaswa kujitathmini je, inaendelea kufanya vizuri katika masuala ya utawala bora. Ilikuwamo kwenye tamko la kiafrika kuhusu wigo wa kwenda Mahakama ya Afrika katika haki za binadamu, lakini imejiondoa.

"Kweli Tanzania, rais akiwa rais miaka mitano, akapata mitano mingine ni kwamba hata awe anakubalika au kupendwa kiasi gani, ibara inasema haikubaliki kuendelea.

"Mchakato wa Katiba kwa sasa si kipaumbele, nchi za Afrika zinapungukiwa na mpishano wa kimawazo kati ya wananchi na viongozi," alisema Kibamba.

Alisema APRM iongeze kasi ya kufanya tathmini na kutolewa ripoti ya kila nchi, ili ikibainika nchi inaendelea kufanya vyema au ina vikwazo vya kusonga mbele kuhakikisha kuna utawala bora.

"APRM imeongezewa majukumu ya SDGs (Mpango wa Maendeleo Endelevu), kuhakikisha Afrika inatekeleza malengo," alisema Kibamba.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, alisema mchakato wa APRM ni muhimu kwa asasi za kiraia, na kwamba kituo hicho kimeandaa mkutano huo ili kufufua majadiliano ya utekelezaji mpango wa APRM.

Balozi Mindi Kasiga, ambaye pia anatoka sekretarieti ya Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Afrika (APRM), akizungumza kwenye mkutano wa pamoja uliokutanisha taasisi mbalimbali, wiki hii, anasema kutokuwapo kwa utawala bora barani Afrika ni kikwazo cha maendeleo.

"Tusisubiri kutoka nje au Umoja wa Mataifa (UN), utuambie hatuna utawala bora, Afrika tujitathmini wenyewe. Utawala bora hauwezi kufanana na nchi za nje, mfano China, Marekani, tufanye juhudi zetu kama Waafrika."



Meneja Mwandamizi wa Chapa ya Coca-Cola Tanzania, Kabula Nshimo (aliyekaa chini kulia), akifurahia jambo na wafanyakazi wa kampuni ya Bonite Bottlers Ltd, mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro juzi, katika uzinduzi wa kampeni inayojulikana 'Maajabu Halisi na Coca-Cola' au 'Real Magic'. Uzinduzi wa kampeni hiyo, unatarajiwa kufanyika katika mikoa mingine ambapo utaambatana na shughuli tofauti za kusisimua zitakazowahusisha wateja na kudumu mpaka kipindi cha msimu wa sikukuu ya Chrismasi na Mwaka Mpya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wasindikaji, wakulima zabibu wapewa mafunzo kuhusu ubora

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

ZAIDI ya wakulima na wasindikaji 100 wa zabibu mkoani Dodoma, wamepatiwa mafunzo yanayolenga kuwaelimisha wadau wote waliopo kwenye mnyororo huo kuongeza thamani ya zao hilo ili kuondokana na changamoto mbalimbali.

Mafunzo hayo yalianza kutolewa Novemba 15 na kumalizika Novemba jana na maofisa wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) katika maeneo ya Dodoma mjini, Hombolo na Mpunguzi jijini Dodoma.

Meneja wa TBS Kanda ya Kati, Nickonia Mwabuka, alisema jana wakati wa kuhitimisha mafunzo hayo kwamba mafunzo hayo yametolewa kuhusu viwango na matakwa ya viwango vya zabibu na bidhaa za zabibu.

Pia alisema mafunzo hayo yalihusu kanuni za kilimo bora, kanuni bora za usindikaji na usafi, teknolojia mbalimbali za usindikaji zabibu na bidhaa za zabibu, usajili wa biashara, ufungashaji na vifungashio na utaratibu wa kuthibitisha ubora wa bidhaa na ushauri kuhusu usafirishaji wa bidhaa kwenda nje ya nchi kuhusiana na masuala ya viwango na ubora.

Alisema mafunzo hayo yametolewa Dodoma kwa kuzingatia kuwa mkoa huo ndio unaolima zao hilo kwa wingi nchini na katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mwabuka alisema walengwa wa mafunzo hayo ni wale ambao wako kwenye mnyororo, yaani wakulima, wasindikaji, wafungashaji wadau wengine ambao wengi ni wajasiriamali wadogo na kati.

"Kundi hili ni sehemu muhimu sana katika sekta hii pamoja na sekta binafsi katika kuchangia pato la taifa, kuongeza ajira na kuondoa umaskini katika nchi yetu," alisema Mwabuka.

Alisema mafunzo hayo yamepokewa kwa mtazamo chanya na washiriki wa mafunzo hayo, kwa kuwa ni mwanzo wa wadau wa zabibu kuwa na mwelekeo mpya na unaozingatia matakwa ya sheria


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

Anwani ya Simu: **"Uvuvi"**
Simu Nambari: +255 (026) 2322612
Nukushi: +255 (026) 2322613
Barua pepe: ps@uvuvi.go.tz
Tovuti: http://www.mifugouvuvi.go.tz

Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Ulinzi,
S.L.P 2847,
**40487 DODOMA.**

**TAARIFA KWA UMMA**

**KUFUNGULIWA KWA MSIMU WA UVUVI WA KAMBAMITI (PRAWNS) KWA MSIMU WA MWAKA 2022**

Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Idara ya Uvuvi inapenda kuwatangazia wananchi wote kwamba uvuvi wa Kambamiti (Prawns) kwa msimu wa mwaka 2022 utafunguliwa tarehe 1 Machi mpaka tarehe 30 Septemba, 2022 kwa Kanda ya Kaskazini (Dar Es Salaam, Tanga, Bagamoyo na Saadani). Aidha, uvuvi huo kwa Kanda ya Kusini (Kisiju, Rufiji delta, Jaja/Kilwa, Lindi na Mtwara) utafunguliwa tarehe 01 Aprili hadi tarehe 31 Agosti, 2022.

Kwa tangazo hili, kila kampuni au mwananchi mwenye nia ya kufanya uvuvi wa kambamiti kwa msimu wa mwaka 2022, anaombwa kutuma maombi kuanzia tarehe 25 Novemba mpaka tarehe 16 Disemba, 2021. Waombaji wanapaswa kuzingatia Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003, Kanuni za uvuvi za mwaka 2009 na marekebisho yake ya mwaka 2020. Aidha, vigezo vya kuzingatia katika maombi ya uvuvi tajwa vinapatikana katika Tovuti ya Wizara (*www.mifugouvuvi.go.tz*) na katika Ofisi za Wizara Kanda ya Dar Es Salaam na Pwani.

Maombi ya leseni za uvuvi wa Kambamiti kwa wavuvi wadogo yatumwe katika Halmashauri husika na wavuvi wakubwa maombi yatumwe kwa Katibu Mkuu-Uvuvi, Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Imetolewa na:

**DKt. Rashid A. Tamatamah**
**KATIBU MKUU-UVUVI**


## Apigia chapuo anwani makazi

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, amesema uwekaji wa anwani za makazi kwenye mitaa utarahisisha kutambua idadi ya nyumba zilizopo.

Mabula alisema hayo jana mjini hapa alipowasili mkoani Kagera kwa ziara ya kikazi na kushiriki uzinduzi wa anwani za makazi kwenye jengo la ofisi za mkoa ikiwa ni kuadhimisha miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika na miaka 59 ya Jamhuri.

Dk. Mabula alisema uwekaji wa anwani hizo lazima uendane na idadi ya nyumba na watu kwenye maeneo na mitaa wanayoishi.

"Siku zote wizara inaitwa nyumba na maendeleo ya makazi lakini leo (jana) hii mtu ukiuliza kuna nyumba ngapi huwezi kusema idadi badala yake kinachoweza kusemwa ni uhitaji wa nyumba kwa mwaka, " alisema Dk. Mabula.

"Sisi wote hapa tunahitaji nyumba zisizopungua milioni tatu unazijengaje? Kwa namna gani? Na lini? Na zitakwemda kuisha lini? hilo linawezekana, " aliongeza.

Pia alisema uwekaji wa anwani utarahisisha maendeleo na kufanya mipango kwenye shughuli zote zinazofanywa na jamii ya watu wanaoshi kwenye maeneo yao.

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Meja Jenerali Charles Mbuge, alisema kwa kufuata maelekezo ya serikali, wataendelea kutoa elimu kwa wananchi ili kutambua umuhimu wa kuwa na anwani za makazi.

"Tukiweka nguvu ya pamoja ufanisi utaonekana na tutakuwa watu wa mfano kwa kuanzisha mpango huu ambao ni msaada mkubwa kwa wakazi wa mtaa na wageni, " alisema Jenerali Mbuge.

**"Siku zote wizara inaitwa nyumba na maendeleo ya makazi lakini leo (jana) hii mtu ukiuliza kuna nyumba ngapi huwezi kusema idadi badala yake kinachoweza kusemwa ni uhitaji wa nyumba kwa mwaka, " alisema Dk. Mabula.**

## Tigo yahamasisha huduma ya malipo kwa njia kidigitali

**Na Mwndishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Tigo, kupitia huduma yake ya Lipa kwa Simu, imezindua promosheni ya mwisho wa mwaka inayoitwa Lipa Kwa Simu, uWini, promosheni.

Kampuni hiyo ilisema jana wakati wa uzinduzi huo mkoani Dar es Salaam kuwa lengo ni kuhamasisha wateja wa Tigo pesa kutumia huduma ya malipo ya kidijitali.

Kupitia promosheni hii watumiaji wote wa Tigo Pesa watapata zawadi za pesa taslimu hadi Sh. 1,000,000, vocha za zawadi na kurudishiwa asilimia 10 watakapotumia Lipa Kwa Simu kulipia bidhaa au huduma kwa wafanyabiashara waliochaguliwa kote nchini.

Ikiwamo ushindi wa milioni 1 kila mmoja kwa wateja kumi watakao kuwa na idadi kubwa zaidi ya miamala ya Lipa kwa simu kwa kipindi kizima cha kampeni. Promosheni ya Lipa Kwa Simu, uWini ilianza jana na itamalizika Januari 7, mwakani.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa promosheni, Ofisa Mkuu wa Huduma za Kifedha Tigo Pesa, Angelica Pesha, alisema promosheni hii inalenga kukuza matumizi ya malipo kidigitali nchi nzima hasa kuelekea kipindi hiki cha sikukuu za Chrismas na Mwaka mpya.

"Tumedhamiria kuwazawadia wateja wetu waaminifu katika msimu huu wa sikukuu kwa kila malipo watakayofanya kupitia huduma ya Lipa Kwa Simu na Tigo Pesa ambapo watapata nafasi ya kujishindia zawadi za fedha taslimu, punguzo la 10% katika maeneo yaliyochaguliwa na zawadi za vocha," alisema Pesha.

"Kila mteja atakayeshiriki atapokea ofa kwa njia ya SMS inayomtaka kufikia idadi au kiwango fulani cha miamala kupitia Lipa Kwa Simu kulingana na wastani wa matumizi yake ya kila wiki, akifikia lengo aliyotengewa mteja atapata zawadi ya Vocha kuanzia Sh. 2,000 hadi Sh. 100,000 kwenye akaunti yake ya Tigo Pesa papo hapo," alisema na kuongeza kuwa wateja 10 bora tu ambao wataongoza kwa kutimiza lengo kwa asilimia 50 watapata zawadi ya vicha ya Sh. 100,000 kila wiki.

Promosheni ya Lipa kwa Simu uWini itawawezesha wateja wote kulipa kwa urahisi kwa makundi mbalimbali ya wafanyabiashara katika sekta zote kama vile sehemu za soko, vituo vya mafuta, migahawa, baa, hoteli, maduka makubwa, maduka ya dawa, maduka ya vifaa na mengine mengi.

Aliongeza mfanyabiashara pia atapata fursa ya kupokea malipo yake kupitia huduma hii ya Lipa Kwa Simu. "Tunawahimiza wafanyabiashara wetu wote kupokea malipo ya kidijitali kutoka kwa wateja wao msimu huu wa sikukuu ili kujijengea nafasi ya kushinda."

# Serikali kupitia upya mkataba wa mgodi wa dhahabu

**Na Marco Maduhu,** KAHAMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Geoffrey Mwambe, amesema serikali inatarajia kupitia upya mkataba wa mgodi wa dhahabu wa Bulyanhulu kuhusu ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami.

Imeelezwa kuwa awali mgodi huo ukiwa chini ya Barrick uliingia mkataba na serikali, kujenga barabara kwa kiwango cha lami kutoka Bulyanhulu wilayani Kahama hadi Mwanza, lakini haukutekelezwa.

Waziri Mwambe alibainisha hayo juzi alipofanya ziara katika mgodi huo wa Bulyanhulu, huku Mbunge wa Msalala wilayani Kahama, Iddi Kasimu, naye akihoji juu ya hatima ujenzi wa barabara hiyo.

Alisema katika makubaliano ya awali na mgodi huo ilikuwa ni kujenga barabara kwa kiwango cha lami kutoka Bulyanhulu wilayani Kahama hadi mkoani Mwanza.

Hata hivyo, licha kuwapo mkataba huo, mpaka sasa hakuna kilichofanyika na kumfanya Waziri Mwambe kutoa ahadi ya kuupitia upya ili kubaini walichokubaliana.

"Mgodi huu ulipokuwa chini ya Accacia ulifanya mambo si mazuri, lakini kwa sasa mkiwa chini ya Twiga naona mnafanya vizuri na hili suala la ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, serikali na nyie tutakaa ili tuone litatekelezwaje," alisema Mwambe.

Katika hatua nyingine, alipongeza mgodi huo kwa kuajiri Watanzania wengi, wakiwamo watu ambao wanaouzunguka pamoja na kuwapatia nafasi za usambazaji bidhaa mbalimbali mgodini hapo.

Awali akizungumza kwenye mgodi huo, Mbunge Kasimu, alisema barabara ya kutoka Bulyanhulu kwenye mgodi huo hadi Kahama yenye urefu wa kilomita 75 ni mbovu.

Aidha, aliomba mgodi huo kutumia mapato yake inayotenga kwa jamii kila mwaka ili kujenga barabara hiyo ili kuondoa kero kwa wananchi.

Naye Meneja uzalishaji dhahabu, wa mgodi huo, Abdalla Kipala, alisema wanatarajia kufunga kazi zao za uzalishaji ifikapo mwaka 2040.

Alisema kabla ya kufikia mwisho wa kufanya shughuli za uchimbaji, watafanya mazungumzo na wilaya ili kuona nini wanaweza kuwafanyia kama wawekezaji.




Ofisa Mkuu wa Huduma za Kifedha Tigo Pesa, Angelica Pesha (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa promosheni ya mwisho wa mwaka inayoitwa Lipa Kwa Simu, uWini. Kulia ni Meneja wa Huduma ya Lipa kwa Simu, Reuben Kamuga na Meneja wa Wateja Maalum wa Tigo Pesa, Mary Rutta. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wachimbaji wadogo sasa kunolewa uchimbaji kisasa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WACHIMBAJI wadogo wa madini ya dhahabu wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wanatarajia kupewa elimu ya uchimbaji wa kisasa na Kampuni ya Sub Gold Limited (SGL), ili kuondokana na uchimbaji holela na kuharibu mazingira.

Aidha, elimu hiyo itakwenda sambamba na utambuzi wa bei halali ya soko la madini katika masoko ya kitaifa kama imeshuka au imepanda, hatua ambayo itasaidia kuondoa malalamiko ya bei kati ya wachimbaji na wanunuzi wa madini hayo.

Meneja wa Kampuni hiyo, Abdurahman Sangey, aliyabainisha hayo wakati akizungumza na vyombo vya habari, ambapo alisema, elimu hiyo itasaidia wachimbaji kutotumia nguvu nyingi wakati wa shughuli za uchimbaji na kuhakikisha wanapata masoko mazuri.

Alisema kwa sasa wachimbaji wamekuwa wakichimba madini kwa kutumia teknolojia ya kizamani, hali ambayo inawafanya kupata madini ya dhahabu kidogo, ukilinganisha na nguvu waliyotumia, hivyo kwa mafunzo hayo yatawabadilisha na kuanza kuchimba kisasa.

Aidha, Sangey alisema, pamoja na kutoa mafunzo hayo kwa wachimbaji wadogo pia watakuwa na suluhisho kubwa la utatuzi wa bei za madini ya dhahabu kwa kuwatafutia masoko katika sehemu mbalimbali hapa nchini na duniani kote.

"Tumeamua kujikita zaidi kutoa elimu ya uchimbaji kisasa kwa kundi hilo kwa sababu uchimbaji wao ni wa kuhamahama na kuharibu mazingira yanayowazunguka na tutashirikiana na Chama cha Wachimbaji Wadogo (TAMIDA) na wataalamu kutoka Wizara ya Madini," alisema Sangey.

Alifafanua mafunzo yatawawezesha wachimbaji kutimiza majukumu yao kwa umakini.

Mmoja wa wachimbaji wadogo kutoka mgodi wa Mwimeilindi, Bundala Masanja, alisema utoaji wa elimu hiyo iende sambamba na elimu ya utunzaji wa kaboni za kukamatia dhahabu ili kutunza mazingira na kuwalinda wananchi wanaozunguka maeneo ya uchimbaji.

Naye Zakaria Mabula alisema, wamekuwa wakiharibu mazingira kwa kuchimba kwa kuhamahama na hii ni kwa sababu wanachimba kwa kubahatisha eneo la madini, na kwamba elimu hiyo itasaidia kuchimba kisasa na kupata madini mengi tofauti na wanavyochimba sasa.

# Waziri: Hivi ndivyo tumejipanga kuliteka soko la mpunga Afrika

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

WAZIRI wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, amesema wizara yake itashirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuanzisha mashamba darasa kwenye zao la mpunga ili kuongeza uzalishaji, lengo kuingia soko la ushindani Afrika.

Amesema kwa sasa katika uzalishaji wa mpunga, wakulima wanapata wastani wa tani mbili kwa hekta moja, lakini nchi nyingine ikiwamo Thailand wakulima wao wanapata tani nane. Prof. Mkenda, alisema hayo alipotembelea kiwanda cha kukoboa na kusindika mchele cha MW Rice Millers Limited kilichoko mjini Morogoro kwa ajili ya kuangalia uzalishaji na kusikiliza vikwazo akiambatana na Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo. Prof. Mkenda alisema lengo la kutoa elimu kupitia mashamba darasa ni kuongeza uzalishaji kutoka tani mbili za mpunga kwa hekta kwenda zaidi hadi kufikia tani tano ili kushindana na mchele unaotoka nchi za nje ikiwamo Pakstani, Thailand na India.

Alisema, ushirikiano huo na TAMISEMI umelenga kuanzisha vituo vya pamoja kwa ajili ya kufanya mashamba darasa kwa wakulima ili kutoa huduma za ugani kwa wakulima wa mpunga ili kuongeza tija katika uzalishaji.

"Tayari tumeshawaandikia wenzetu wa TAMISEMI ili kuainisha maeneo yatakayoanzishwa hayo mashamba darasa," alisema. Alisema nia ni kutoa elimu hiyo inayotokana na Kiwanda cha MW Rice Millers Limited kuelezea kikwazo upatikanaji wa mpunga kutoka kwa wakulima na hivyo kushindwa kuongeza masoko.

Waziri Mkenda, alisema kiwanda hicho kinakusudia kuongeza uzalishaji zaidi na kuuza katika nchi nyingi zaidi, hivyo kutoka na kikwazo hicho, lazima uzalishaji wa mbunga uongozeke nchini.

Alisema pia kiwanda hicho kimeomba kuwapo kwa vituo vya ukusanyaji wa mpunga kutoka kwa wakulima ili kuwarahisisha kufikisha kiwandani kitu ambacho Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na TAMISEMI wameahidi kushughulikia kwa haraka.

Ofisa Rasilimali Watu wa kiwanda hicho, Deoudedith Kikuna, alisema endapo serikali itawasaidia kutatua vikwazo, wataongeza uzalishaji kutoka tani 288 za mchele zinazozalishwa kila siku kuongezeka mara tatu zaidi. Alisema wapo katika mpango wa kuongeza uzalishaji kutokana na mahitaji makubwa ya masoko ya ndani na nje kutokana na ubora wa bidhaa hiyo.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhandisi Robert Gabriel (kulia), akipokea msaada wa madawati 100 kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano kutoka Benki ya Exim, Stanley Kafu, kwa ajili ya kusaidia kuondoa adha ya upungufu wa madawati katika shule mbalimbali za msingi mkoani humo, ikiwa ni sehemu ya mpango wa benki hiyo wa ugawaji wa madawati 1,000 katika mikoa mbalimbali hapa nchini kupitia mpango wake wa kusaidia jamii ujulikanao Exim Cares. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwanza yapigwa jeki madawati

**Na Mwandishi Wetu**

MKOA wa Mwanza umepunguziwa tatizo la uhaba wa madawati kwa ajili ya shule, baada ya kukabidhiwa madawati 100.

Madawati hayo yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 20 yemetolewa na Benki ya Exim Tanzania kwa ajili ya kusaidia kuondoa adha ya upungufu wa mawadati katika shule mbalimbali za msingi mkoani Mwanza.

Akizungumza jana kwenye kukabidhi madawati hayo kwa uongozi wa Serikali mkoani Mwanza, Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano kutoka Benki ya Exim, Stanley Kafu, alisema hatua hiyo itasaidia kuboresha mazingira kwa wanafunzi kupata elimu.

Aidha, alibainisha kuwa benki hiyo inaadhimisha miaka 24 tangu kuanzishwa kwake mwaka 1997, ambapo katika kusherehekea maadhimisho hayo, imeanzisha mpango wa kutoa madawati 1,000 kote nchini ikiwa ni sehemu ya kurejesha shukurani kwa jamii.

"Miezi miwili iliyopita tulisherehekea miaka 24 tangu benki yetu ianze kutoa huduma ambapo tuliamua kutoa madawati 1,000, ili kwa kushirikiana na serikali tusaidie kupunguza changamoto za elimu nchini. Tunashukuru Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliuzindua mwezi uliopita mkoani Lindi, hivyo tuko hapa kukabidhi madawati haya 100 ikiwa ni sehemu ya kutekeleza mpango huo," alisema Kafu.

Akipokea madawati hayo, Mkuu wa Mkoa Mwanza, Mhandisi Robert Gabriel, aliipongeza benki hiyo kwa kutimiza miaka 24 tangu kuanzishwa kwake na kuamua kurejesha fadhila kwa jamii kupitia madawati hayo kwani yatasaidia kuondoa uhitaji uliopo na kuboresha mazingira ya wanafunzi kujifunza.

"Madawati haya yataleta mageuzi makubwa kwenye mkoa wetu kwani uhitaji ni mkubwa, tuna miradi mingi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa inayoendelea baada ya kupokea fedha nyingi kutoka kwa Rais Samia Suluhu Hassan hivyo natoa shukurani za dhati kwenu na naomba taasisi nyingine ziige mfano huu," alisema Mhandisi Gabriel.

Akipokea madawati hayo kutoka kwa Mkuu wa Mkoa Mwanza, Mkuu wa Wilaya Misungwi, Veronica Kessy, alisema kwa kushirikiana na viongozi wenzake atahakikisha madawati hayo yanakabidhiwa katika shule zenye uhaba na kutunzwa vyema kwa lengo la kuleta tija iliyokusudiwa hususani kukabiliana na uhaba uliopo uliotokana na mwitikio wa wazazi kupeleka watoto shule kutokana na sera ya elimu bila ada. Naye Ofisa Elimu Mkoa Mwanza, Mwalimu Martine Nkwabi, alisema kwa shule za msingi na sekondari kuna uhaba wa takribani madawati 180,000 na kuongeza kuwa madawati 100 yaliyotolewa na Benki ya Exim yatasaidia kukabiliana na uhaba huo huku yakiwasaidia wanafunzi 300 kuwa na mazingira bora ya kukaa wakiwa darasani.

# TADB, KCBL kuwapatia wakulima wadogo bil. 2/-

**Na Mwandishi Wetu**

WAKULIMA wadogo mkoani Kilimanjaro wamepata fursa ya uwezeshwaji, baada ya Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kuingia katika makubaliano na Benki ya Ushirika Kilimanjaro (KCBL) kuwakopesha shilingi bilioni mbili kwa riba nafuu.

Lengo la mkopo huo ni kukuza biashara na kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo, ufugaji na uvuvi.

Makubaliano haya, yaliyosainiwa jana mjini Moshi, yataiwezesha TADB kutoa dhamana kwa wakulima wa mkoani Kilimanjaro watakaoenda kuomba mikopo KCBL kufanya shughuli za kilimo, ufugaji pamoja na uvuvi kwa riba nafuu. Dhamana hii inaratibiwa na TADB chini ya Mfuko Maalum wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo nchini 'SCGS'.

"Kwa muda mrefu tumeona wakulima wetu nchini wakipata changamoto ya mitaji. Wengi wakilazimika kukopa kwa riba za kibiashara ambapo wengi wao wamekuwa wakipata changamoto ya kuhimili riba hizo kubwa. Hivyo, kama taasisi ya maendeleo ya kifedha, kupitia mfuko wa dhamana kwa wakulima wadogo, tumeona umuhimu wa kutoa mikopo hii nafuu kwa kushirikiana na KCBL ili kuwawezesha wakulima wengi zaidi katika kanda ya kaskazini, kupata mitaji," alieleza, Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Frank Nyabundege.

Mkuu wa Wilaya ya Moshi Mjini, Said Mtanda, aliwapongeza KCBL na TADB kuingia katika ushirikiano huo.

Godfrey Ng'urah, Meneja Mkuu wa KCBL, alisema kiwango hicho cha mkopo kitaenda kuongeza uzalishaji mara mbili katika shughuli za kilimo mkoani humo, ikiwamo uzalishaji wa pembejeo, upatikanaji wa matreka na mengineyo.

# Dentsu yazindua wiki ya masoko

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Masoko Kidigitali na Mawasiliano ya Dentsu Tanzania, imezindua wiki ya masoko kwa lengo la kuwawezesha wataalamu wa fani ya masoko, mawasiliano na mahusiano kuzibainisha na kuzitumia fursa zilizopo kwenye fani hiyo nchini.

Wiki hiyo itafanyika kwa siku tatu kuanzia Desemba mosi hadi 3, mwaka huu, ambapo pia kutakuwa na mijadala itakayoshirikisha wadau wa fani hizo kujadili njia nzuri za kufanya kazi kwenye fani hiyo.

Mkurugenzi wa Dentsu Aegis Network Tanzania, Edward Shila, alisema kwa sasa matumizi ya data yamekuwa ni muhimu na yanatumika zaidi katika kutengeneza mazingira bora ya ufanisi wa kazi kwenye fani mbalimbali, hivyo hata kwenye fani ya masoko data zilizopo zinaweza kutumia katika kutengeneza mpango kazi mzuri wa shughuli za masoko na mawasiliano na kuzitumia vema fursa zinazopatikana.

Shilla aliyashukuru mashirika na kampuni za TBL, LAS Consultancy, Eskimi, We media na infocus studio ambao waliwafadhili kwa ukarimu kufanikisha tukio hilo.

Makandarasi maji wanavyoitibua Sekretarieti ya CCM


Ukurasa 12


Ukurasa 13

# siasa

JUMATANO NOVEMBA 24, 2021
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe

**Bunge la Tanzania na dhana za kuhoji 'utakatifu, udhaifu'**

RUSHWA VS UCHAGUZI

# Wadau: Ya ngono inachafua wanawake kisiasa

## ■Waungana na Warioba kutaka nayo ikomeshwe

**Na Sabato Kasika**

WAKATI Tanzania inaelekea kwenye jubilei ya miaka 60 ya Uhuru, kada mbalimbali zinazungumzia maendeleo ya taifa tangu mwaka 1961 hadi sasa na kuibua changamoto zilizopo.

Miongoni mwao ni Waziri Mkuu mstaafu, Jaji Joseph Warioba, ambaye anajikita kwenye siasa na kutahadharisha kuwa rushwa katika uchaguzi imekuwa kubwa na kushauri ikomeshwe.

Ni katika kipindi cha Dakika 45 cha ITV katika kutathmini miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania, anaposema, rushwa inaonekana waziwazi, kwamba mtu anayetaka uongozi siku hizi analazimika kuwa na fedha na kutumia fedha.

Mwanasiasa huyo mkongwe anasema, bila fedha, hawezi kupata uongozi, hali ambayo inasababisha rushwa iendelee kuenea na kuonya kuwa ipo kwenye siasa hasa wakati wa uchaguzi na haijakomeshwa.

"Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa TAKUKURU ilianzishwa ili kupambana na rushwa, hasa kubwa, na siku za nyuma chombo hicho kilifanya kazi vizuri, lakini sasa kimebaki kupewa amri na viongozi," Jaji Warioba anasema.

Anaeleza kushangaa jinsi ambavyo chombo hicho kinatumika kama Jeshi la Polisi kwa kupewa maagizo, hakiwezi kuchunguza viongozi na kwamba ndiyo maana siasa za rushwa zinaendelea nchini bila hatua zozote kuchukuliwa.

"Ifike wakati sasa viongozi wakubali kuna rushwa, iko ndani ya uongozi, kinachotakiwa ni kuwekwa utaratibu wa kuishughulikia ndani ya viongozi na wenyewe wakikubali kupambana nayo itaisha," anasema.

**RUSHWA HII TISHIO**

Nancy Mrikaria, ni Katibu Mkuu wa zamani wa Chama cha TLP, anaungana na Jaji Warioba kuhusu saratani ya rushwa katika uchaguzi, lakini anajikita zaidi kwenye rushwa ya ngono.

"Rushwa ya ngono katika uchaguzi ipo, baadhi ya wanawake wanaotaka uongozi kupitia vyama vyao huombwa, ila husita kuweka wazi, vitendo hivyo, labda kwa sababu ya aibu, lakini sisi wadau tunaendelea kuelimisha jamii kuikataa kwani inadhalilisha utu wa mwanamke," anasema Nancy.

Imekuwa ni kikwazo kwa wanawake kupata uongozi, na kwamba wapo wanaofanikiwa kutokana na uwezo wao wa kuongoza na wengine wanaangukia kwenye rushwa hiyo ya ngono, anaeleza.

"Vilevile, wapo wanaokubali kutoa ngono wakapata uongozi, wengine pamoja na kushiriki ngono hawapati nafasi na baadhi wanajiweka kando na siasa kuepuka mtego huo," anasema.

Anasema, ni vyema wadau wa siasa wakaendelea kupaza sauti kupinga rushwa zote katika uchaguzi na TAKUKURU ichukue hatua dhidi ya wanaolalamikiwa.

"Rushwa ya ngono ipo, kwani nimehudhuria semina nyingi zinazoandaliwa na majukwaa ya wanawake na kusikia malalamiko hayo, hivyo nayo inatawala katika siasa za Tanzania hasa wakati wa uchaguzi," anaeleza.

**WOTE WAWILI WABANWE**

Mwanasheria Felix Mkosamali anakumbusha kuwa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Mwaka 2007, inagusa pande mbili, kwa mtoaji hadi kwa mpokeaji, na kwamba ni kati ya sheria muhimu katika kupambana na rushwa.

"Rushwa ni adui wa haki" hivyo ni muhimu kujua kuwa kutoa na kupokea rushwa ni jinai, ni vyema Watanzania wakalijua hilo kuwa kosa la rushwa halihusu upande mmoja tu," anasema Mkosamali.



Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Salum Hamdun. **PICHA: MTANDAO**

Katika ufafanuzi wake, anasema, mtoa rushwa na anayeipokea wanapochunguzwa na kubainika kuhusika na vitendo hivyo, wanatakiwa kufikishwa mahakamani.

Mkosamali mbunge wa zamani wa Muhambwe mkoani Kigoma - NCCR-Mageuzi , anasema ni muhimu kila mtu kutambua kuwa kutokujua sheria si utetezi iwapo atatenda kosa lolote.

"Nimpongeze mzee Warioba kwa msimamo wake wa ukweli na uwazi, hamung'unyi maneno, akiona jambo haliko sawa, hasiti kusema, ingawa hakugusia kuwa hata mpokea rushwa ana makosa," anasema.

Mwanasheria huyo anafafanua kuwa, Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa imeainisha makosa kadhaa ya rushwa ambapo mtu akitenda, mchakato wa uchunguzi na mashtaka ya rushwa utaendeshwa dhidi yake.

"Kwa ujumla sheria hii imeainisha makosa 14 ya rushwa yanayojitokeza kwa taswira mbalimbali. Kwa mfano wa makosa ya rushwa ni kama ifuatavyo; kupokea rushwa, kushawishi au kulazimisha kupewa rushwa," anasema.

Anaongeza kuwa kutoa rushwa au kuahidi kutoa rushwa, adhabu yake ni faini ya Sh. 500,000 hadi Sh. milioni moja au kifungo kati ya miaka mitatu hadi minne ama faini na kifungo kwa pamoja.

"Kutoa au kupokea rushwa ili kupata mkataba wa kutoa huduma kwa idara ya umma au shirika la umma, adhabu ni faini ya Shilingi 1,000,000 hadi tatu au kifungo kati ya miaka mitatu hadi mitano ama faini na kifungo kwa pamoja," anasema.

Anataja rushwa ya ngono kwamba mtu mwenye mamlaka kutumia madaraka kulazimisha au kushawishi mwengine kufanya naye tendo la ngono kwa ahadi ya kumpatia ajira au upendeleo fulani, adhabu ni faini ya Sh. 5,000,000 au kifungo kisichozidi miaka mitatu ama vyote kwa pamoja.



Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka (wapili kushoto), na viongozi wengine wa CCM, wakikagua mradi wa maji wa Ziwa Tanganyika. **PICHA: BEATRICE SHAYO**

# Makandarasi maji wanavyoitibua Sekretarieti ya CCM

■ Shaka aiibua TAKUKURU uchunguzi, Chongolo kuja na kiini

**Na Beatrice Shayo aliyekuwa, KIGOMA**

WAKATI taifa likiteseka kwa ukame na uhaba wa maji, wakuu wa Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, wakiwa mkoani Kigoma wamekutana na kilio cha wananchi wakilalamikia makandarasi kutokamilisha miradi.

Wanakerwa na kutotekeleza miradi huku wengine wakikimbia kazi zao na kuwaachia watu mateso mathalani ukosefu wa maji kwenye mradi wa Ziwa Tanganyika.

Ziara hiyo iliyoanza katikati ya mwezi huu ikiongozwa na Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, inafanyika Kagera, Geita, Kigoma, Katavi na Bukoba.

Ziara inalenga kuimarisha uhai wa chama mashinani na kukagua utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 - 2025, kama inavyoelekezwa na Halmashauri Kuu ya CCM Taifa iliyokutana Juni mwaka huu.

Wanaojumuika na Katibu Mkuu Chongolo ni Naibu Katibu Mkuu wa CCM - Bara, Christina Mndeme, wengine ni Makatibu wa NEC Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, Siasa na Uhusiano wa Kimataifa, Ngemela Lubinga na Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana wa CCM (UV-CCM), Kennan Kihongosi.

Viongozi hao wanalakiwa na malalamiko ya makandarasi kuchelewesha miradi na kushindwa kukamilika kwa wakati na wengine kufanyakazi chini ya kiwango licha ya kulipwa.

**SHAKA ATAKA UCHUNGUZI**

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Shaka Hamdu Shaka, inaitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kuchunguza Wizara ya Maji kwa kitendo cha makandarasi kutimka na kuacha kazi za ujenzi.

Shaka akiwa mkoani Kigoma, alipotembelea mradi wa kitekeo cha maji wa Ziwa Tanganyika chenye uwezo wa kuzalisha lita milioni 42 kwa siku, anatoa maelekezo hayo.

Anasema katika maeneo aliyotembelea makandarasi wamejitoa na kusababisha miradi kukwama huku wananchi wakipata shida ya maji na huduma nyingine.

Anasema kuna haja ya TAKUKURU kuchunguza kitendo cha makandarasi kujitoa katika miradi ya maji ili kuepuka miradi kuchelewa kukamilika kwa wakati.

Katika kandarasi ya Ziwa Tanganyika tayari mkandarasi alijitoa kufanya kazi akiwa amefanya upembuzi yakinifu na kukubali kufanya kazi, Shaka anasema.

"Hapa sasa mtu mmoja kashajitoa na huyu aliyepo ni wa pili, hii ni shida kubwa ya makandarasi kuondoka niliongea na Waziri wa Maji, Juma Aweso, akaniambia anakusudia kukutana na makandarasi nchi nzima nadhani hili nalo ni muhimu," anasema Shaka.

Anaongeza kuwa wanawapa kazi makandarasi wa nchini kwa kuwaamini, matokeo yake wanawarudisha nyuma kwa kitendo cha kujitoa katika miradi kabla ya kuikamilisha.

Aidha, Shaka anasema kwa sasa jicho la chama hicho litakuwa katika mradi wa maji wa ziwa Tanganyika kuona namna gani utekelezaji wa ahadi ya Rais Samia Suluhu Hassan unatekelezeka kwa kuhakikisha watu wanapata maji.

**TATIZO GEITA**

Christine Mndeme, Naibu Katibu Mkuu CCM Bara aliyetembelea Wilaya ya Nyang'wale mkoani Geita, anakutana kisa cha mkandarasi ambaye kwa kipindi cha miaka mitano hajakamilisha ujenzi wa jengo la halmashauri.

Akizungumzia suala hilo, anasema kitendo hicho kimesababisha Mkurugenzi wa Halmashauri kuendelea kufanya kazi katika jengo la utawala la hospitali huku serikali ikiwa imetoa fedha kwa ajili ya ujenzi huo usiokamilika.

"Jengo la utawala leo lina miaka mitano halijakamilika na kunasababisha matatizo makubwa kwa mkurugenzi na timu yake. Wanakaa kwenye jengo la hospitali fedha ya ujenzi ipo na pochi la mama limefunguka lakini kuna tatizo la mkandarasi," anasema Christina.

Anasema mkandarasi amekuwa akifanya uzembe haonekani kazini na ukienda hakuna watumishi au ni wachache na kusababisha kero kwa mkurugenzi kwa sababu hana ofisi na wananchi wanapata kero ya kukosa huduma.

Naibu Katibu Mkuu wa CCM, anasema watumishi hao wanatumia jengo la utawala la hospitali ambalo hutumika kutoa huduma kwa wananchi.

"Mkandarasi hajanipa majibu ya kuridhisha kaniambia hawezi kuendelea kujenga mpaka apatiwe fedha na hawezi kupatiwa fedha nyingine ni mpaka amalize kipande kile... ndipo alipwe fedha nyingine huyu hatufai. Mkandarasi mshauri ni mtu binafsi naye hamshauri mwajiri ambaye ni halmashauri ya wilaya hiyo. Hatuwezi kuendelea na uzembe huu kama imeshindikana atupishe tutafute mkandarasi mwingine mwenye uwezo," anasema Naibu Katibu Mkuu Bara.

Anapokakagua ujenzi wa jengo hilo la Halmashauri ya Mlale, anasema CCM haitosita kuiagiza serikali kuvunja mikataba ya makandarasi wanaoshindwa kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wakati.

"Sijaridhishwa na kazi ya mkandarasi mshauri wa kampuni ya BICCO. Hajatekeleza majukumu yake ya kulinda fedha za serikali zinazotumika katika ujenzi huu," anaonya.

Anaongeza: "Chama kinaagiza mradi huu ukamilike kwa wakati na hakitosita kuishauri serikali kuvunja mkataba kama mkandarasi anafanyakazi zake kwa kusuasua."

Mndeme amwagiza mkandarasi anayejenga jengo hilo kampuni ya SUMA JKT kuongeza kasi kwa kuleta nguvu kazi ya kutosha.

Anautaka uongozi wa halmashauri kuandaa taarifa yenye usahihi kuhusu kiasi halisi cha fedha kilichotumika katika mradi huo baada ya kubaini ukakasi katika takwimu za fedha zilizotengwa.

"Mradi huu mmenieleza unagharimu Sh. bilioni 2.8, mkataba mpya na SUMA JKT unagharimu Sh. bilioni 2.1, mmelipa mkandarasi TBA Sh. milioni 499 ambaye mkataba wake umevunjwa," anasema.

"Lakini hapa kuna bilioni moja ambazo halmashauri imetenga kwa ajili ya mradi huu, nataka kujua hizi fedha matumizi yake ni yapi? Hizi ni pesa za serikali, hivyo lazima matumizi yake yafahamike," Christina anasisitiza.

Baada ya kukosekana majibu hayo, anaagiza kuandaliwa ripoti yenye usahihi wa matumizi ya fedha halisi za mradi huo ambao tangu mwaka wa fedha 2016/2017 hadi sasa bado haujakamilika.

Aidha, anawataka makandarasi washauri kutekeleza majukumu yao kwa maslahi ya nchi badala ya kufumbia macho vitendo vinavyoashiria miradi ya ujenzi kwenda kinyume cha matakwa ya kimkataba.

> "Hapa sasa mtu mmoja kashajitoa na huyu aliyepo ni wa pili, hii ni shida kubwa ya makandarasi kuondoka niliongea na Waziri wa Maji, Juma Aweso, akaniambia anakusudia kukutana na makandarasi nchi nzima nadhani hili nalo ni muhimu," anasema Shaka.

**MAKANDARASI NI KERO**

Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, akitoa ya moyoni anasema hawawezi kukubaliana na uzembe unaofanywa na makandarasi na kuahidi kulifanyia kazi suala hilo kwa kuangalia kwa kina kiini chake.

Anasema iwapo wakibainika ni kipi kiini cha tatizo serikali itachukua hatua.

Hawawezi kuwa na taasisi za serikali au zenye uhusiano na taasisis za umma ambazo zinafanya mambo ovyo na kuchelewesha maendeleo halafu watendaji wakazichekea, akisisitiza kuwa hayupo tayari katika hilo.

"Ninakwenda kuangalia na nitalifanyia kazi lazima tutafute matokeo. Fedha zimeletwa wewe ndiye uliyekubali kujenga hujafikia kiwango unachotakiwa kulipwa unataka pesa, hiyo fedha inatoka wapi bila kutimiza matakwa ya malipo? Hilo halikubaliki ni lazima tuende mbele tuambiane ukweli," anasema Chongolo.

Chongolo anasema kuna umuhimu wa mikataba iwekewe vipengele vitakavyowezesha kuifuta pale mkandarasi anapobainika amekiuka makubaliano kuliko kutumia muda mrefu kuuvunja huku miradi ikikwama na wananchi wakiteseka.

UCHAMBUZI

# Bunge la Tanzania na dhana za kuhoji 'utakatifu, udhaifu'

**Na Deogratias Mutungi**



Bunge kwenye moja ya vikao vyake jijini Dodoma. **PICHA: MTANDAO**

NENO "utakatifu" linachukuliwa mara nyingi au kuhusishwa na Mwenyezi Mungu. Ni sahihi, lakini linaweza kutumiwa kuendana na masuala mengine kulingana na muktadha.

Utakatifu unatokana na neno la Kiebrania "qadash" likimaanisha kujitenga au kutengwa kwa usafi, aidha katika Kigiriki hujulikana kama "hagios" ikiwa na maana kutokuwa na makosa, udhaifu au uchafu.

Hivyo utakatifu unamaanisha kukaa mbali na uchafu au udhaifu na katika siasa, bunge ni muhimili wa dola unaoweza kuhusishwa na utakatifu kiutendaji na kuisimamia serikali kikamilifu.

Utakatifu unatumiwa kulingana na muktadha na kwenye hoja hii bunge ni jumba la dhahabu lenye heshima ya pekee katika kusimamia maendeleo ya nchi na raia wake.

Linapaswa kujiendesha na kujisimamia kitakatifu, linalofanya kazi kwa hoja zenye mrengo chanya wa ukombozi wa taifa kiuchumi, kisiasa na kijamii, likiwa ni baraza lenye watakatifu wanaoisaidia nchi kutunga sheria na kuisimamia serikali katika utekelezaji wa majukumu yake bila woga, hofu wala upendeleo na kuipitisha bajeti yake.

Baadhi ya watu hulichukuliwa bunge kama jumba la kuvuna na kugawana mapesa ya walipa kodi hivyo kuliondolea utakatifu.

Swali hapa ni kwa kiwango gani wabunge wa Afrika na Tanzania wanautendea haki utakatifu katika kutatua matatizo ya wananchi na kutimiza wajibu wao kwa serikali kadiri majukumu yao yanavyoelekeza kikatiba?

Dhana ya utakatifu inasimamia usafi, uimara na ubora wa viongozi wa kisiasa kama wabunge katika kutimiza wajibu wao ndani ya nchi ili kuleta maendeleo ya kweli kwa wananchi kama walivyoahidi wakati wa kuomba kura na kula kiapo cha utumishi.

Ifahamike wazi kuwa duniani kote mabunge ni chemichemi, nembo na taswira ya taifa kwa ubora na umadhubuti wa watu wake.

Bunge dhaifu huzalisha mifumo dhaifu ndani ya taifa lake, na huo ndiyo mwanzo wa serikali legelege, mikataba tata, mifumo duni na vitu vyake vyote huwa dhalili na huko ndiko kupoteza utakatifu wake pale linaposhindwa kujenga hoja za kisiasa zenye fikra tunduizi (critical thinking) na kuwa na uwakilishi wenye tija kwa umma.

Bunge na wabunge wake ni chombo kitakatifu pale linapoonyesha utimamu wa kutimiza majukumu yake ipasavyo na si kwa matakwa ya mihimili mingine au maslahi ya yeyote.

Mkataba wa ndoa ya bunge ni baina ya wabunge watakatifu na wananchi wao, hivyo ni lazima utakatifu uwe wa kufungamana na maslahi ya wapigakura.

Utakatifu wa bunge ni kutambua umuhimu uliopo baina yake na wananchi katika kupigania maslahi ya watu wa tabaka la chini, ndiyo mama na mkombozi wa dhuluma, ufisadi, uminywaji wa haki ya aina yoyote ya kunyanyasa wanyonge na raia.

Bunge la Tanzania lipo kwa mujibu wa katiba na sura ya tatu, vifungu 62,63, 64 na 65 sambamba na vifungu vyake vidogo. Kimuundo kuna maelezo yanayojitosheleza kuutambulisha mhimili huo wa bunge na majukumu yake kwa umma.

Hoja ya kuwapo udhaifu ndani ya mhimili huu wa dola si jambo la kawaida kama watu wengi wanavyodhani. Ni suala gumu linalohitaji ushahidi wa kutosha kabla ya kulituhumu, bunge linapoyumba na kudhoofu.

Bunge la Tanzania ni takatifu, kwa sababu iwapo ni dhaifu taifa lingeyumba kwani ni sawa na uti wa mgongo unapojeruhiwa bila shaka mwili utakosa ushirikiano na viungo vingine ikibidi hata kupooza.

Mara nyingi hatima yake ni mauti, kadhalika udhaifu wa bunge ni umauti wa nchi na watu wake, hivyo wanaojenga hoja ya udhaifu wa bunge la taifa hili wanautambua udhaifu huo, au ni udhaifu upi unaosemwa? Bila shaka ni ule wa kusadikika.

Inawezekana wapo wanaojenga hoja ya udhaifu wanakosea, hata hivyo kukosea kwa mara ya kwanza si dhambi, dhambi ni kueleweshwa na wasikubali kuelewa, Waswahili wana usemi usemao "kutenda kosa si kosa bali kulirudia".

Inawezekana wapo wanaojenga hoja ya udhaifu wanakosea, hata hivyo kukosea kwa mara ya kwanza si dhambi, dhambi ni kueleweshwa na wasikubali kuelewa, Waswahili wana usemi usemao "kutenda kosa si kosa bali kulirudia".

Kwa ujumla Bunge la Tanzania si dhaifu ni imara, kwa sababu ni chombo kinachojiendesha kwa mujibu wa kanuni zake zilizotungwa ndani ya bunge hilo mahsusi kwa ajili ya kusimamia shughuli zake.

Aidha, bunge huikosoa serikali na kutunga sheria za kuendesha nchi kulingana na utaratibu wa bunge ulivyo, swali linakuja ni lini bunge lilishindwa kutimiza wajibu wake wa kuikosoa serikali?

Wapo wabunge watakatifu kwa maana ya qadash" na "hagios" wanaojenga hoja na kuisahihisha serikali na taasisi zake kwa uchungu mkubwa kwa maslahi ya umma. Hata wakitaka bajeti kuongezwa na mambo kadhaa wa kadhaa kupewa umuhimu.

Yapo maazimio ya bunge katika kuwajibisha watendaji wa serikali na taasisi za umma zinazolegalega kiutendaji au kutuhumiwa kwa ufisadi wa mali za umma, kuhujumu uchumi na kukosekana uwajibikaji.

Wapigakura wameshuhudia wabunge wakiwajibisha mawaziri, watendaji mbalimbali, wakiunda kamati zinazofichua uozo kwenye madini, nishati, fedha lakini pia ndani ya kamati za maadili wakiwahoji watendaji na wabunge watovu wa nidhamu.

Bunge ni mahala patakatifu waliomo ni watakatifu, hivyo ni vyema kujenga hoja zenye dira na mwelekeo wa kisiasa unaolenga kukosoa kwa maslahi ya nchi na watu wake na inapoonekana kuna upungufu isichukuliwe kana kwamba bunge ni dhaifu.

Misimamo binafsi na hoja za mbunge kupelekea watu kutoa hukumu kwa bunge zima kuwa ni dhaifu kwa sababu ya kusigana na kutokubali mawazo ya mtu mmoja hakumaanisha kuwa chombo hicho si kitakatifu.

Tanzania inalo bunge imara lenye utashi wa kuwajibika, kuisimamia na kuikosoa serikali kwa mujibu wa katiba na maslahi ya umma. Bunge ni chombo kitakatifu kinachohudumia umma kulingana na dhamana waliyopewa na wapigakura wao.

**dmutungid@yahoo.com**
**0717718619**

# NANA AKUFO ADDO

## Rais Ghana anayeonekana kioo cha kuing'arisha Afrika…ingawa anazungukwa na makandokando

**Na Mwandishi Wetu**

JANUARI 2017, wakili wa zamani wa haki za binadamu, mwanadiplomasia Nana Akufo-Addo, aliapishwa kwa mara ya kwanza kuwa rais mpya wa Ghana, katika uchaguzi uliofanyika Desemba mwaka 2016.

Rais Akufo Addo, alimshinda mpinzani wake John Dramani Mahama, katika uchaguzi wa vyama vingi uliokuwa unawachuanisha wapinzani hao wa jadi ambao mara nyingi wanagombea urais wa nchi hiyo.

Akufo Addo anatokea Chama cha Patriotic Party [NPP], ikiwa ni mara yake ya nne kugombea na kushindwa bila kukata tamaa. Ni jasiri aliyezaliwa Machi 29, mwaka 1944.

Rais huyo ni mwanasiasa mkongwe asiyechoka na alipotangazwa mshindi anatamba "taifa hili sasa ni mwenge wa demokrasia Afrika Magharibi na bara zima" akiahidi kukabiliana na uchumi uliozorota, suala ambalo alilitilia mkazo wakati wote wa kampeni na hicho ndicho anachokifanya sasa.

Anawatangazia wafuasi wake kuwa ushindi wake ni hatua anayoifurahia sana katika maisha yake yote na kuahidi kuwa atafanya kila juhudi kuhakikisha kuwa anatekeleza matakwa ya wananchi wa Ghana.

Baada ya kuingia Ikulu ya jijini Accra, Akufo Ado, mwaka 2019 alitajwa kuwa kiongozi bora barani Afrika na watatu duniani.

Kwanza taasisi ya utafiti ya 'Canadian Leaders of Tomorrow', ilimtaja Addo kuwa ni kiranja bora wa Afrika kufuatia kura zilizopigwa kwa kusimamiwa na shirika hilo.

Akufo-Addo, aliibuka kuwa Rais bora kuanzia mwaka 2018 na kuripotiwa na taasisi na mitandao ya nchi hiyo.

Lakini si Canada pekee, utafiti kama huo uliofanywa nchini Marekani na Shirika la World Vision Forum, linamweka Addo juu ya marais wote wa Afrika likimtaja pia kuwa ni watatu kati ya viongozi mashuhuri na bora duniani wenye maono na fikra pevu.



Rais Nana Akufo-Addo wa Ghana, anayesifiwa kwa umahiri. **PICHA: MTANDAO**

### NINI KINACHOMPAISHA

Kwa mujibu wa Shirika la Canadian Leaders of Tomorrow, tangu achukue uongozi mwaka 2017 kutoka kwa John Mahama, Akufo-Addo amejidhihirisha kuwa ni 'Mtu wa Watu' mwenye kutekeleza sera yakinifu (za uhakika na kweli) zikiwamo kutoa elimu bora ikiwamo ya sekondari na kujitolea kwake kwenye miradi na mipango ya maendeleo ya Ghana na kupambana kikamilifu na kutokomeza rushwa jambo linalomweka juu ya kilele cha mafanikio.

Baadhi wanaotajwa kumkaribia Addo Akufo wameondoka madarakani, lakini waliopo ni pamoja na Danny Faure wa Seychelles na wa Gambia Adama Barrow, nao wanaelezwa kuwa ni miongoni mwa viongozi tano bora wa Afrika.

Ghana ya Akufo Addo ni nchi inayosifiwa kwa demokrasia thabiti, ambayo vyama vya upinzani vinashinda na kuongoza dola.

Tena, Ghana imekuwa na mabadiliko saba ya madaraka kwa njia ya amani tangu kurudi kwa demokrasia zaidi ya miaka 30 iliyopita na katika taifa hilo malalamiko ya baada ya uchaguzi yamekuwa yakishughulikiwa kupitia mahakama jambo ambalo ni nadra katika nchi nyingi za Afrika.

Rais Akufo Addo, anasifika kuiongoza vyema Ghana, anayoelezwa kuwa tangu achukue nchi mwaka 2016, taifa hilo limerekodi ukuaji wa hali ya juu wa uchumi na maendeleo mengine wakati wa kipindi cha kwanza cha madarakani wakati alifanya kazi kubadilisha uchumi unaotegemea sana uuzaji nje wa kakao na hivi karibuni mafuta na dhahabu.

Ghana inasifika kwa kuweka mikakati ya maendeleo inayojumuisha sekta zote kwa mfano sekta ya viwanda, ulinzi wa mazingira afya na usalama kazini.

> Kwanza taasisi ya utafiti ya 'Canadian Leaders of Tomorrow', ilimtaja Addo kuwa ni kiranja bora wa Afrika kufuatia kura zilizopigwa kwa kusimamiwa na shirika hilo.

Utawala bora ndiyo ngao ya kuhakikisha maendeleo endelevu kwa taifa hilo, lakini serikali inajizatiti kupunguza tofauti za kiuchumi huku ukilenga kutoa huduma bora za kijamii, kuongeza usalama kazini na kazi bora kwa wafanyakazi, elimu bora na kuwa na miji bora na salama.

Akufo-Addo amepata tuzo kadhaa ikiwamo ya kutambua mchango wake kwenye kutetea haki za binadamu ya Mother Theresa Memorial International Award for Social Justice.

Aidha, ni mshindi wa Tuzo ya Rais Bora wa Afrika mwaka 2018 (African Best President Award). Mwaka jana kiongozi huyo wa Ghana alitajwa kuwa Rais Bora wa Afrika.

### UKOSOAJI UPO

Ghana inachukuliwa kuwa moja ya mataifa yaliyo na utulivu zaidi katika kanda ya Afrika Magharibi na Afrika kwa ujumla tangu kurejeshwa kwa mfumo wa demokrasia ya vyama vingi nchini humo mwaka 1992.

Kiongozi wao wa Chama cha NPP, anakosolewa kuwa licha ya kujizolea sifa na kuibuka mshindi baada ya kujizolea asilimia 51.59 ya kura zilizopigwa kwenye uchaguzi wa hivi karibuni mwaka 2020.

Wengi wanauchukulia kama ushindi kwa Ghana. Hiyo ni kwa sababu, nchi hiyo kwa mara nyingine, imeendesha uchaguzi wa amani bila wapigakura kuchoma nyumba na kuuana mambo ambayo mara nyingi huonyesha namna uchaguzi wa Afrika ulivyo.

Au, kuwa sahihi zaidi, inamaanisha kwamba vifo na uharibifu uliotokea Ghana havikuwa vingi ikilinganishwa na nchi nyingine barani Afrika. Kwa hayo, Ghana imeendelea kushikilia nafasi ya kinara wa demokrasia Afrika.

**MITANDAO**

# Serikali yaombwa maofisa ugani maeneo ya vijijini

**Na Peter Mkwavila,** KONGWA

SERIKALI imeombwa kuwa na mpango wa kuajiri maofisa ugani kwa ajili ya kukabiliana na upungufu uliopo katika maeneo ya vijijini.

Pia imeshauriwa iendelee na jitihada za kuwawezesha maofisa ugani vitendea kazi kama usafiri ili waweza kuwafikia wakulima wengi na kwa muda mwafaka.

Ushauri huo ulitolewa juzi wilayani hapa na Ofisa Kilimo Mkuu kitengo cha usimamizi wa mazingira Wizara ya Kilimo, Evelyn Kagoma, kwenye mafunzo ya maofisa ugani na wakulima kuhusu utabiri wa hali ya hewa na ushauri kwa ngazi ya wilaya kwa msimu wa 2021/2022.

Kagoma alisema serikali inapaswa kuweka mpango wa kuwaajiri maofisa ugani ili kupunguza uhaba uliopo huko vijijini ambako ni mkubwa.

Aidha, alisema serikali inatakiwa kuona umuhimu wa ununuzi wa vitendea kazi kwa maofisa ugani hao ambavyo vitakavyo wawezesha kufanya kazi kwa ufanisi kwa kuwafikia wakulima kwa haraka.

"Vijiji vilivyo vingi vipo kwenye maeneo ya mbali, hivyo wakipatiwa huduma hizo itakuwa rahisi kuwafikia kwa wakati na kutekeleza majukumu yao kwa urahisi tofauti na jinsi ilivyo kwa hivi sasa," alisema.

Ofisa huyo aliwashauri wakulima kutumia kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi ambacho kina mbinu na teknolojia kulingana na kilimo ikolojia.

Aidha, alishauriwa kulinda na kutunza mazingira kwa ajili ya maendeleo endelevu kwa kuepuka kulima kwenye vyanzo vya maji, kujiepusha na uchomaji moto misitu ovyo na kutumia viuatilifu bila kufuata maelekezo ya watengenezaji.

Mtaalamu wa hali ya hewa kutoka Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Mponda Malozo, aliesema taarifa za hali ya hewa kwa wakulima na wafugaji ni muhimu katika shughuli za kilimo na ufugaji kwa kuwa zimekuwa zikitegemea mvua.

Alisema taarifa hizo zitasaidia kuandaa kalenda ya shughuli za kilimo kwa wakati na zitatumia teknolojia sahihi za kilimo kwa msimu husika.



Mtaalamu wa Hali ya Hewa kutoka Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Mponda Malozo (kushoto), akikabidhi majarida ya mwongozo kwa ajili ya elimu ya kilimo na ufugaji kwa maofisa ugani na wakulima kwa Ofisa Ugani wa mkoa wa Dodoma, Wilfred Mofule, wakati wa mafunzo yaliyofanyika, wilayani Kongwa, mkoani humo juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## CBE kuanzisha kozi za mtandao

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Prof. Emanuel Mjema, amesema katika mwaka wa masomo 2021/22 katika kampasi ya Dodoma wamepanga kuanzisha fani mbalimbali za masomo ikiwamo utoaji wa kozi kwa njia ya mtandao.

Prof. Mjema aliyasema hayo wakati wa mahafali ya 56 ya chuo hicho na kuongeza kuwa hatua hiyo ni katika kutekeleza mkakati wa kutanua wigo wa kutoa huduma na kuongeza fani mbalimbali za kitaaluma.

"Chuo katika kampasi ya Dodoma kimejipanga kuendelea kutanua wigo kwa kutoa huduma zake na kuongeza fani mbalimbali za kitaaluma katika ubora wa hali ya juu na katika kufanikisha lengo hili katika mwaka wa masomo 2021/22 CBE tumeanzisha kozi kadhaa katika mwaka wa masomo 2021/22 kuanzia ngazi ya astashahada hadi shahada ya kwanza," alisema.

Prof. Mjema alizitaja kozi hizo kuwa ni kozi ya Masoko kwa njia ya kidigitali, Utalii na Usimamizi wa Matukio, Uongozi wa Biashara katika nyanja ya rasilimali watu, Utunzaji wa Kumbukumbu na Nyaraka, Uhasibu na Kodi, Uhasibu na Fedha, Benki na Fedha ambazo zitatolewa kuanzia angazi ya astashahada hadi shahada ya kwanza.

Alisema pia CBE inaendelea kutoa kozi za muda mfupi za bodi mbalimbali za kitaaluma kama vile kozi za wakaguzi kiwango cha kati na kiwango cha mwisho, kozi na Bodi ya Ununuzi na Ugavi sambamba na kozi za fani mbalimbali zinazoendana na sekta ya biashara.

Aidha, Prof. Mjema alisema pia chuo kinatarajia kuzindua kampasi nyingine Zanzibar hivyo kufanya CBE kuwa na jumla ya kampasi tano ambazo ziko Kanda ya Mashariki, Kanda ya Kati, Kanda ya Ziwa na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

"Chuo cha Elimu ya Biashara kilianzishwa mwaka 1965 kikiwa na wanafunzi 28 katika kampasi moja ya Dar es Salaam na miaka 18 baadaye yaani mwaka 1983 kampasi ya Dodoma ilifunguliwa huku mwaka 2007 ilianzishwa kampasi ya tatu jijini Mwanza ikiwa ni miaka 42 baada ya kuanzishwa chuo hicho na mwaka 2013 ikaanzishwa kampasi ya Mbeya," alisema.

Prof. Mjema alisema pia chuo kimeendelea kuboresha namna ya utoaji elimu kwa kufanya maboresho mbalimbali ya miundombinu na vifaa na kuzindua kanuni za kufundisha za uanagenzi na atamizi kwa ajili ya kuwafundisha wanafunzi kwa vitendo.

Alisema chuo kimekuwa mastari wa mbele kutumia wataalamu wake katika kuunga mkono juhudi za serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan za kuendeleza azma ya Hayati John Magufuli ya kuhamishwa makao makuu ya serikali katika Jiji la Dodoma.

"Chuo kimekuwa kikifanya makongamano ya kitaaluma ya kitaifa kila mwaka kutoka mwaka 2019/20 na kwa mwaka huu tumeendesha kongamano la kitaifa lililokuwa na kaulimbiu isemayo 'Ukuaji wa Uchumi Shirikishi kwa Maendeleo Endelevu.

"Hii ni hatua mahususi ya kuhusiana wataalamu katika nyanja za biashara na uchumi na katika Kongamano hilo wanazuoni wa ndani na nje ya nchi waliopata fursa ya kuwasilisha matokeo ya utafiti wao," alisema.

## Samia kufungua mkutano wa taasisi za fedha

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kufungua mkutano wa 20, wa Taasisi za Fedha nchini utakaofanyika kwa siku mbili jijini Dodoma kuanzia kesho.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Idara ya Uhusiano wa Umma na Itifaki ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT), lengo la mkutano huo ni kujadili uimarishaji wa uchumi wa Tanzania kufuatia janga la UVIKO-19.

"Mkutano huo ambao umeandaliwa na Benki Kuu ya Tanzania kwa kushirikiana na Umoja wa Benki Tanzania (TBA), unatarajiwa kuhudhuriwa na washiriki takribani 300 kutoka taasisi za fedha, sekta binafsi, serikali, mashirika ya kimataifa, taasisi za elimu, asasi za kiraia na vyombo vya habari," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Aidha, katika mkutano huo jumla ya mada nne zitawasilishwa na wataalamu waliobobea kutoka ndani na nje ya nchi. Mada hizo ni ukuaji wa uchumi endelevu wakati na baada ya janga la UVIKO -19, vipaumbele na sera mbadala, kuchochea kasi ya maendeleo ya kidijitali katika kuimarisha ukuaji endelevu wa uchumi.

Mada nyingine ni sarafu za kidijitali, uzoefu, vihatarishi, usimamizi na kuongeza mikopo kwa sekta binafsi baada ya janga la UVIKO-19, wajibu wa serikali, taasisi za fedha na sekta binafsi.

"Mada hizo zimechaguliwa kuendana na hali ya sasa, ambapo uchumi wa dunia unaendelea kuimarika kufuatia athari za janga la UVIKO-19, na kuongezeka kwa matumizi ya teknolojia za kidijitali na fedha za mtandaoni, kwa mujibu wa taarifa hiyo.



# Mbaroni utekaji madereva pikipiki wakiwa wamevalia sare za JWTZ

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linawashikilia watu wawili kwa tuhuma za kuteka madereva wa pikipiki maarufu 'Bodaboda' na kuwapora vyombo vyao, huku wakiwa wamevalia sare za Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ).

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, aliwataja watuhumiwa hao ni Muganyizi Leopord (36) na Majaliwa Mwashiuya (31), mkazi wa Songea katika Mamlaka ya Mji wa Tunduma mkoani Songwe.

Alisema Novemba 21, mwaka huu, watuhumiwa walimteka mchimba madini, Goodluck Andengulile (22) mkazi wa Matundasi wilayani Chunya na kumpora pikipiki yake yenye namba za usajili MC.810 CCH na kutokomea nayo.

Alisema watuhumiwa walimvizia Andengulile kwenye msitu wa Mbiwe uliopo katika Kata ya Makongolosi wakati akirejea nyumbani saa 11:30 alfajiri na kumpora pikipiki kisha wakatokomea nayo huku wakiwa wamevalia magwanda ya jeshi.

Kamanda Matei alisema kufuatia tukio hilo, makachero wa Jeshi la Polisi walianza kuwasaka watuhumiwa hao na ndipo walipowakamata wakiwa hawajatoka katika mipaka ya Wilaya ya Chunya.

"Wakati watuhumiwa wakipekuliwa Leopord alikutwa na cheti cha Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) chenye namba za usajili AD.9664 SM na ilibainika kuwa alimaliza mafunzo ya JKT Juni 25, 2009 katika kikosi cha Kanembwa JKT kilichoko mkoani Kigoma," alisema Kamanda Matei.

Alisema watuhumiwa walikiri kuhusika kwenye tukio la kumpora Andengulile pikipiki na kwamba wanaendelea kuhojiwa ili kubaini matukio mengine waliyoshiriki.

Kamanda Matei alisema watuhumiwa watafikishwa mahakamani baada ya upelelezi wa shauri hilo kukamilika na kwamba washirika wa watuhumiwa hao wakibainika watashughulikiwa pia.

Aliwataka wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo ili kutokomeza vitendo vya uporaji na mauaji ya madereva bodaboda katika mkoa huo.



Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheli Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Fredrick Shoo (kulia), akifurahia jambo na Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vincent Anney (katikati) pamoja na Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Bendera Mkondora (kushoto), alipokwenda kusuluhisha mgogoro wa kuhamisha makao makuu ya Dayosisi ya Konde kutoka Tukuyu kuipeleka jijini Mbeya hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Homera atoa siku 30 soko lililotelekezwa lifanye kazi

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ametoa siku 30 kwa viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali kuhakikisha soko la mchele la kimataifa la Igurusi lililojengwa kwa mabilioni ya fedha linaanza kufanya kazi.

Alisema kwamba lengo ni lisaidie kuboresha bei ya mpunga wilayani humo.

Alimtaka Mkuu wa Wilaya hiyo kwa kushirikiana na halmashauri hiyo kukutana na uongozi wa Mtandao wa Vikundi vya wakulima Tanzania (MVIWATA) ili wajadiliane na kuweka mipango ya namna ya kuliendesha soko hilo.

Homera alisema soko hilo limejengwa kwa zaidi ya Sh. bilioni mbili na lilikamilika kwa zaidi ya miaka saba iliyopita, lakini mpaka sasa halina tija kutokana na kwamba limetelekezwa na wakulima hawapeleki mchele wao kwenda kuuza kwenye soko hilo.

Alisema soko hilo kwa sasa limekuwa kama limetelekezwa jambo ambalo serikali haiwezi kuvumilia kutokana na fedha ambazo zilitumika kwenye ujenzi wake.

"Ni lazima hili soko lianze kuleta tija inayostahili, kwa sasa halmashauri haipati chochote na wakulima wetu hawanufaiki, nataka ndani ya mwezi mmoja hili soko lianze kutumika na lilete tija," alisema Homera.

Awali Diwani wa Kata ya Igurusi, Hawa Kiwele, alisema soko hilo limetelekezwa kwa muda mrefu na hakuna hata mtu mmoja anayehangaika nalo na kwamba kwa sasa limebaki kama gofu kutokana na kutotumika.

Alisema wafanyabiashara hawalitumii na badala yake mchele unauzwa barabarani na kwenye mashine za kukoboa mpunga jambo ambalo alidai kuwa siyo sahihi.

"Soko lilijengwa kwa viwango mpaka huduma za kifedha zipo, lakini halitumiki kabisa, hata miundombinu yake haiboreshwi hivyo tunakuomba Mkuu wa Mkoa utusaidie maana hili soko kwa sasa linachukuliwa kiwepesi sana," alisema Kiwele.

Baadhi ya wakulima wa mpunga katika wilaya walisema kinachowakwamisha kwenda kuuza mchele kwenye soko hilo ni gharama za usafirishaji kutoka mashineni kwenda kwenye soko hilo.

Joyce Asajile alisema kwa sasa bei ya mchele kwenye mashine za kukoboa mpunga ni Sh. 20,000 kwa debe, lakini wakisafirisha kwenda kuuza kwenye soko hilo bado wanauza kwa bei hiyo hiyo.

Alisema wafanyabiashara wa mchele huwa wanalazimika kuuzia mashineni ili kupuka gharama za usafirishaji huku wengine wakikwepa tozo zingine za kwenye soko hilo ambazo zilipangwa na wamiliki wa soko.

Aliiomba serikali ikiwezekana iweke utaratibu ambao utawalazimisha wafanyabiashara wa mchele kwenda kuuzia mchele wao kwenye soko hilo badala ya kuuzia kwenye maeneo ambayo siyo rasmi kwa kazi hiyo ikiwamo mashineni na barabarani.

Vilevile, aliiomba serikali iwatafutie wanunuzi wa mchele ambao watanunua bidhaa hiyo kwa kiwango kikubwa na waelekezwe kwenda kununulia kwenye soko hilo badala ya kwenda kwenye mashine kama ilivyozoeleka.

# Wanakijiji wachangishana fedha ujenzi wa barabara

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WAKAZI wa Kijiji cha Kilambo, kilichoko Kata ya Mwatenga katika Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wameanza kuchangishana fedha kwa ajili ya kujenga barabara ili kuwaepusha wanafunzi na vifo vitokanavyo na kusombwa na mafuriko wanapoenda shuleni kipindi cha masika.

Kijiji hicho kinakabiliwa na tatizo la ubovu wa barabara hasa kipindi cha mvua tangu nchi ilipopata uhuru mwaka 1961, hali ambayo imekuwa ikiathiri sekta mbalimbali ikiwamo afya, elimu na shughuli zingine za kiuchumi na wamekuwa wakitumia punda kubeba wagonjwa.

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa kamati ya ujenzi wa barabara ya kijiji hicho, Tatizo Jamson, alisema wananchi wake wameamua kuchangishana fedha hizo ili kuokoa maisha ya watoto wao wanaosoma Shule ya Msingi Kilambo.

Alisema wakati wa masika maji huwa yanajaa barabarani hali ambayo huwa inasababisha vifo vya wanafunzi kwa kusombwa na maji huku wakiwa hawapati msaada wowote kutoka serikalini.

"Barabara yetu haijawahi kulimwa na greda tangu nchi yetu ipate uhuru, hali hiyo imesababisha barabara hii kuwa korongo kubwa kama unavyoona, huwa linajaa maji wakati wa mvua na kukata mawasiliano kabisa," alisema Jamson na kuongeza:

"Mwaka jana wanafunzi wanne walikufa baada ya kusombwa na mafuriko walipokuwa wakienda shuleni kupitia kwenye korongo hilo, ndio maana mwaka huu wananchi wameamua kuchanga fedha ili tulete greda la kuinua tuta kabla mvua haijaanza kunyesha."

Alisema wananchi hao wamechangishana zaidi ya Sh. milioni 9.3 ambazo zinatumika kukodisha greda la kuinua tuta ili serikali ipange bajeti ya kujenga barabara hiyo.

Baadhi ya wananchi wa kijiji hicho walisema waliamua kuchanga fedha kutokana na adha ambayo wamekuwa wakiipata wakati wa mvua ambapo maji hukwamisha shughuli zao za maendeleo pamoja na kusababisha vifo.

Mmoja wa wananchi hao, Feston Sagutangu alisema kutokana na ubovu wa barabara hiyo wananchi huwa wanashindwa kusafirisha mazao yao kutoka mashambani kwenda sokoni pamoja na kusafirisha pembejeo za kilimo kupeleka mashambani.

Vilevile, alisema baadhi ya wazazi huwa wanatumia muda mwingi kuwasindikiza watoto kwenda na kurudi shuleni hali ambayo inashusha hata uzalishaji mali kwenye maeneo yao.

"Tunaamini serikali itakuja itusaidie, hii barabara yetu ina zaidi ya Km 40, lakini kwa fedha tulizochangishana zitatusaidia eneo dogo sana na sisi hatuna utaalamu wowote ndio maana tunataka kuinua tuta kuelekea shuleni tu," alisema Sagutangu.

Hivi karibuni, Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema barabara hiyo imetengewa bajeti ya zaidi ya Sh. milioni 200 na kwamba itaanza kujengwa hivi karibuni na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA).

Aliwataka wananchi hao kuvuta subira wakati serikali ikijiandaa kujenga barabara hiyo, ambapo alisema ni miongoni mwa barabara muhimu kwa maendeleo ya wananchi wa wilaya hiyo.





## Othman ashtukia uharibifu mazingira

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amewaagiza watendaji na mamlaka zinazohusika na usimamizi na matumizi ya mawe kutengeneza utaratibu utakaowezesha maeneo yaliyochimbwa rasilimali hiyo kurekebishwa na kutumika kwa shughuli zingine zikiwamo za kiuchumi.

Othman aliyasema hayo jana Pujini, Chakechake, kisiwani Pemba alipotembelea eneo la Kwareya Pujini lililoharibika vibaya kwa kuchimbwa kifusi akiwa katika mfululizo wa ziara ya kutembelea maeneo mbalimbali kisiwani Pemba kuona uharibifu wa mazingira uliofanywa na shughuli za binadamu na mabadiliko ya tabia nchi.

Alisema Zanzibar ina ardhi ndogo na kwamba ni lazima baada ya kufanyika matumizi ya uchimbwaji wa kifusi kuhakikisha utaratibu maalum unatumika ili pasibakie kama palivyoharibiwa.

Kwa mujibu wa Othman, suala la kulinda na kuhifadhi mazingira haliihusu mamlaka inayosimamia mazingira pekee bali ni la kila mmoja miongoni mwa wananchi na taasisi za serikali, hivyo ni lazima kushirikiana katika kuhakikisha madhara yatokanayo na uharibifu wa mazingira hayaongezeki Zanzibar.

Alisema kwa kuwa Zanzibar ina ardhi ndogo, haitakuwa busara eneo lililotumika kuwa ardhi iliyotupwa na badala yake juhudi na mpango maalum uandaliwe ili kunusuru hali hiyo kuendelea.

Pia alisema si jambo la busara kwamba juhudi za maendeleo zinazofanyika zikasababisha uharibifu mkubwa wa mazingira bila mamlaka na taasisi kuchukua tahadhari na kuaandaa utaratibu bora utakaosaidia kupunguza madhara yatokanayo na matumizi ya rasilimali hiyo.

Aliwataka watendaji kufahamu kwamba suala hilo halihitaji kukumbushwa na viongozi wakuu wa serikali, hivyo ni vyema wananchi kujiunga na taasisi za serikali kujenga utamaduni wa kuwa na mkakati wa pamoja utakaosaidia kuirejesha rasilimali hiyo baada ya matumizi yaliyofanyika.

Alishauri watendaji kupanga na kutambua kwamba gharama za ujenzi wa barabara zinajumuisha pia gharama za kurekebisha baada ya kufikiri na kuandaa mkakati, na utaratibu wa pamoja ili jukumu hilo lisitupwe kwa taasisi fulani kwa kuwa janga la kimazingira ni la Wazanzibari wote.

# SMZ yatoa tamko kuungua hoteli

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) imesema imeathirika kwa kukosa mapato kutokana na kuungua moto kwa hoteli nne za kitalii katika eneo la Jambiani, Mkoa wa Kusini Unguja.

Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Lela Muhamed Mussa, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, mjini hapa. Hoteli hizo ziliteketea kwa moto Novemba 19, mwaka huu, majira ya saa 11:00 jioni.

Alisema wafanyakazi 148 walioajiriwa katika hoteli hizo, ajira zao zimesimamishwa kutokana na hasara kubwa walizopata wamiliki.

"Ninaomba nichukue nafasi hii kutoa mkono wa pole kwa uongozi wa hoteli za Villa De Coco, Fun Beach, Spice Island na Kobe kwa kuungua na moto ambao inasemekana umesababishwa na hitilafu ya majiko ya gesi," alisema Waziri Lela.

Aliusihi uongozi wa hoteli hizo kuwa wastahimilivu katika kipindi hiki kigumu na kuvitaka vyombo vinavyohusika kutekeleza majukumu yao kikamilifu, ili kubaini chanzo hasa cha maafa hayo, ili kuendelea kujenga imani kwa wawekezaji wa sekta ya utalii kuendelea kuekeza nchini.

Akizungumza baada ya kuzikagua na kuwafariji wamiliki wa hoteli hizo, Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, alisema serikali itatoa kila aina ya ushirikiano katika kurudisha hadhi ya hoteli hizo.

Makamu huyo aliziagiza mamlaka na taasisi zinazohusika na masuala ya sekta ya utalii kukaa pamoja na kuwa na mapendekezo ya kuishauri serikali yatakayosaidia kurudisha hali za hoteli hizo.

Aliwataka wawekezaji hao kujenga imani kuwa serikali imeguswa na kadhia hiyo na itatoa ushirikiano wake katika kuwasaidia wawekezaji waliopatwa na athari.

Katika hatua nyingine, Hemed alizitaka mamlaka zinazohusika na utoaji wa huduma kwa wawekezaji kuendelea kutoa taaluma juu ya miundombinu bora ya kutumia katika ujenzi wa hoteli ili kuepukana na majanga.

Pia aliupongeza uongozi wa serikali za mkoa na wilaya kwa hatua za haraka ulizochukua katika kukabiliana na janga hilo kwa kuwa hakuna taarifa yoyote iliyoripotiwa ya majeruhi wala kifo.

Akitoa taarifa kuhusiana na janga hilo, Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadidi Rashid, alisema, hoteli hizo zimeteketea kwa moto uliosababishwa na kuungua kwa sehemu ya jiko katika hoteli ya Villa De Coco.

Hadidi alisema moja ya changamoto zilizojitokeza ni kukosekana kwa miundombinu bora ya kupambana na moto, hivyo kuishauri serikali kuangalia namna nzuri ya kuimarisha miundombinu hiyo ikizingatiwa kuwa mkoa wa Kusini Unguja ni ukanda wa uwekezaji wa hoteli za kitalii.

Alibainisha kuwa kutokana na tukio hilo, bado thamani halisi ya hasara iliyopatikana hajifahamika na wahusika wanaendelea na tathmini.

Nao wamiliki wa hoteli hizo, waliishukuru serikali kwa jitihada zake kwa kushirikiana nao katika uokoaji wa wageni waliokuwapo katika eneo la tukio.

Waliomba serikali kungalia jinsi ya kuwasaidia na hasara iliyopatikana kwa kuwa ni kubwa na ikizingatiwa kwa kipindi kirefu sasa hawakufanya biashara kutokana na wimbi la ugonjwa wa corona.



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, akifungua maji kutoka kwenye tangi la mradi wa kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua baada ya kupokea mradi huo kwa niaba ya serikali kutoka kwa Mkurugenzi Mkaazi wa UNESCO Tanzania, Tirso Das Santos (hayupo pichani), katika Shule ya Kisiwa Panza, Kisiwani Pemba juzi. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Vijana 10,000 wabainika kutumia mihadarati Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ZANZIBAR inakadiriwa kuwa na vijana zaidi ya 10,000 ambao wamo katika matumizi ya dawa za kulevya na hadi mwishoni mwa mwaka jana watu ambao wako katika nyumba za upatikanaji nafuu wa dawa za kulevya ni 349.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Mkuya Salum, mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Migombani, mjini hapa kuhusu mwaka mmoja wa Rais Dk. Mwinyi wa uongozi wake kupitia wizara hiyo.

Alisema katika kuimarisha udhibiti wa dawa za kulevya mitaani, jumla ya kilogramu 94.573 za dawa hizo zimeteketezwa Zanzibar.

Waziri aliitaja mitaa hatarishi kwa matumizi ya dawa za kulevya kuwa ni Kikwajuni, Segea, Kidongo Chekundu, Miembeni, Chuwini, Jang'ombe, Migombani, Nungwi, Makunduchi na maeneo ya Mji Mkongwe kwa Unguja na Pemba ni Chakechake, Pujini na Wete.

Alisema kuna ongezeko la matukio 52 ya ukamataji na matukio 393 ya dawa za kulevya yameripotiwa kwa kipindi cha Januari hadi Septemba, mwaka huu, ikilinganishwa na matukio 341 yalioripotiwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka jana.

Waziri alisema matukio hayo yamesababisha kukamatwa kwa kilogramu 8.5 za heroine na kufunguliwa kesi 168 sawa na ongezeko la kesi 19 ikilinganishwa na mwaka uliopita ambapo gramu 761 za heroine zilikamatwa na kufunguliwa kesi 149.

"Jumla ya kilogramu 189.3 za bangi zilikamatwa na kufunguliwa kesi 220 sawa na ongezeko la kesi tano ikilinganishwa na mwaka uliopita ambapo kilogramu 39 za bangi zilikamatwa na kufunguliwa kesi 189 na gramu 180 za mirungi zilikamatwa na kufunguliwa kesi tano. Pia gramu 191 za skanka zilikamatwa na kufunguliwa kesi mbili," alisema Dk. Mkuya.

Pia alisema tayari rasimu ya sheria mpya ya udhibiti wa dawa za kulevya imeandaliwa na inatarajiwa kuwasilishwa katika kikao kijacho cha Baraza la Wawakilishi.

Alisema sheria hiyo itawezesha Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Dawa za Kulevya kuwa na nguvu kisheria za kupambana na dawa za kulevya.

Alisema kupitia sheria hiyo, kutakuwa na maabara ya pamoja ambayo itahakikisha inabaini uhalifu mapema zaidi na kuwa na kikosi maalum ambacho kitakuwa na kazi ya kusimamia udhibiti wa uhalifu huo pia kufupisha muda wa usikilizaji wa kesi za dawa za kulevya.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**SPORAH JOHN MWANKOSOLE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1787-0060** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia ILOMBA SEKONDARI mwaka 2014. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya Polisi: **DAR/CEN/RB/260675/2021.**

1165683602

## KUPOTEA KWA VYETI



**ANETH ASAJILE** anatangaza kupotelewa na vyeti,cha kidato cha nne chenye index namba **S.2395-0010** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya KIWIRA mwaka 2012 na cheti cha kuresit kidato cha nne index namba **P.0461/0001** kupitia kituo/shule ya secondary JOHN PAUL mwaka 2019 na result slip ya kidato cha sita yenye index namba **P0461/0502** iliyotolewa kupitia kituo/shule ya secondary ya JOHN PAUL mwaka 2021,yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi, **DOD/DOD/RB/509924/2021**

1165843602

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**SALOME J. MLOWE**

anatangaza kupotelewa na kadi ya gari iliyokuwa na namba ya usajili **T 965 BZE** yenye chasis namba **NCZ200059936** na engine namba **1NZFEB390677.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Taarifa ya Polisi: **IRI/IRI/RB/555911/2021**

1165839002

## UNCLE MO ENTERPRISES LTD

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

TUTAFANYA MNADA TAREHE 27/11/2021 SAA NNE ASUBUHI WA KUUZA **NYUMBA ILIYOPO NDACHI SOUTH, PLOT NO. 2 BLOCK 'A' MALI YA BWANA ABDALLAH OMARY KAPILIMA,** BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIYOKOPA **UHUMA FINANCIAL SERVICES, P.O. BOX 11058 DODOMA.** MNADA UTAFANYIKA NYUMBA ILIPO, HIVYO TUNAPENDA KUWATANGAZIA WAHITAJI WOTE.

**KWA MAWASILIANAO PIGA NO. 0717417520/0754303498.**

1165838002

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJ

**ABEL MHINA MWETA** wa SLP Manundu, Korogwe, anatangaza kupoteza kadi ya pikipiki ya miguu mitatu (Bajaj) aina ya TVS King yenye namba **MC 172 AQS,**
Yenye Chassis NO. **MD6M14PKXD4H12815.**
Taarifa ya kupotea kwa kadi hiyo imetolewa Kituo cha Polisi Korogwe Novemba 22, 2021, na kupewa Loss Report **KOR/RB/657/2021.**

---

**JAMHURi YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**FORM II**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya mwanzo MAKOLE**

**Usimamizi wa mirathi NA. 104/2021**

**Ombi la HABIB MAZAHER LALJI kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu MAZAER HUSSEIN JAFFER LALJI**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII POPOTE ALIPO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 03-12-2021 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 22/11/2021

SAHIHI YA HAKIMU

116583702

---

**IN THE HIGH COURT OF UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**TEMEKE HIGH COURT SUB – REGISTRY**
**(ONE STOP JUDICIAL CENTRE)**
**AT TEMEKE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 36 OF 2021**

**In the Matter of the Estate of the Late FERDINAND JOSEPH MPANDUJI**

**and**

**In the Matter of Application for Letter of Administration of the Late FERDINAND JOSEPH MPANDUJI DECEASED OF DAR ES SALAAM**

**By OIGENIA FERDINAND MPANDUJI....................PETITIONER**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to the above-named petitioner. Objections to the grant should be filed on or before the 8th day of December, 2021.
Dated at this 18th day of November, 2021.

DEPUTY REGISTRAR

116580702

***Uza,***

***Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza***

***Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## CCM yaahidi kupinga ukatili wa kijinsia

**Na Beatrice Shayo,** TABORA

NAIBU Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Christina Mndeme, amewahakikishia wanawake nchini kuwa chama kitaendelea kulinda haki za wanawake pamoja na vitendo vya ukatili.

Mndeme aliyasema hayo jana wakati akizungumza katika kikao cha shina namba tatu Kijiji cha Lumbe, Wilaya ya Kaliua, Mkoa wa Tabora.

Katika kikao hicho, wajumbe wa shina hilo wakati wa kujadili ajenda ya ulinzi na usalama, walieleza kuibuka kwa matukio ya wanaume kuwapiga wake zao hadi kuwadhalilisha.

"Kumpiga mwanamke ni ushamba na si ujasiri. Mwanamke ukipigwa nenda kashtaki dawati la jinsia ili haki itendeke. Serikali ya CCM itaendelea kuwalinda na kuwakinga wanawake dhidi ya vitendo vya udhalilishaji," alisema.

Mndeme aliwataka wajumbe wa shina hilo pamoja na wazee kukemea vitendo hivyo na kusisitiza maadili ndani ya jamii.

Kadhalika, aliwataka wanaume ambao wana malalamiko kuhusu kunyanyaswa na wake zao, wakashtaki katika madawati ya jinsia badala ya kulalamika pekee. Akiwa katika kikao hicho cha shina, baadhi ya wananchi waliibuka wakidai kuondolewa katika maeneo ya hifadhi ya misitu na mapori ya akiba kinyume cha sheria.

Mndeme alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Kaliua, Paul Chacha, kutoa ufafanuzi kuhusu madai hayo na mkuu huyo kuwataka watu hao kueleza ukweli mbele ya kiongozi na si uongo.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameamua Kijiji cha Lumbe ambacho kilikuwa ndani ya eneo la hifadhi, wananchi waendelee na shughuli zao na tayari ametoa Sh. milioni 60 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa matatu. Pia alisema eneo linalojengwa zahanati nalo lilikuwa ndani ya hifadhi lakini sasa eneo hilo liko nje ya hifadhi.

"Hawa wanaosema wameondolewa katika maeneo yao waseme ukweli. Hata wazee wa kijiji hiki wanafahamu kwamba hao si wenyeji wa Kijiji cha Lumbe ni wavamizi. Walivamia maeneo ya msitu, wakakata miti na huko ndiko yakawa maficho ya vikundi vya kihalifu," alisema.

Chacha alisema baadhi ya wavamizi hao, wakishirikiana na raia wa kigeni, walikuwa wakijishughulisha na matukio ya uporaji mnadani, mauaji na wizi wa mifugo.

# Watakiwa kuhuisha milki ardhi

**Na Munir Shemweta,** KAGERA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amewahimiza wamiliki wa ardhi kuhuisha milki zao zilizoisha muda ili kuepuka kufutiwa ardhi wanayomiliki kwa mujibu wa sheria.

Sheria ya Ardhi Na 4 ya mwaka 1999 inamtaka mmiliki wa ardhi kuhuisha milki yake baada ya muda wa awali aliopewa kwisha. Mmiliki huyo anatakiwa kuomba kuongezewa muda wa kumiliki ardhi na mamlaka husika ina wajibu wa kumwongezea au kutomuongezea kulingana na masharti ya umiliki ambayo ni pamoja na kufanya maendelezo katika eneo analomiliki.

Akizungumza na watendaji wa sekta ya ardhi na wananchi waliowakabidhi hati za ardhi juzi, kwenye ukumbi wa Manispaa ya Bukoba, Naibu Waziri Mabula alisema watendaji wa ardhi wanatakiwa kuangalia namna ya bora ya kuwafikia wale wote ambao hati zao za umiliki ardhi zimeisha muda.

Naibu Waziri alisema katika Manispaa ya Bukoba, kuna milki takriban 22 zimeisha muda na wamiliki wake bado hawajajitokeza kuhuisha na kuwataka watendaji wa ardhi kwenda eneo hilo kuwakumbusha ili kuhuisha milki zao.

Pia aliwataka watendaji wa ardhi kuhakikisha wanatoa elimu kwa wamiliki wa ardhi kuhusiana na umuhimu wa kuhuisha milki zao zilizokwisha muda na kufafanua kuwa kutofanya hivyo kutasababisha mmiliki hizo kufutwa.

"Kama umepewa hati ya miaka 33 au 69 halafu muda wake umeisha na wengi wenye hati za aina hiyo muda wake umwekwisha, unatakiwa kuihuisha hati na usipofanya hivyo ardhi unayomiliki anaweza kupatiwa mmiliki mwingine na hatua hiyo inaweza kuleta manung'uniko wakati uamuzi umefanyika kisheria," alisema.

Naibu Waziri Mabula aliwataka watendaji wa sekta ya ardhi kutotumia fursa ya kuisha muda wa umiliki kuwanyang'anya wamiliki maeneo yao na badala yake wahakikishe wanatoa elimu ya kuhuisha sambamba na kufuata sheria wakati wa kutekeleza sheria.

Baadhi ya wananchi wa Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera walitaka kuwapo utaratibu wa kuwakumbusha wamiliki ardhi kuhuisha hati zao pale muda unapokuwa umeisha ili kuepuka milki hizo kufutwa bila wao kujua.

Diwani wa Katerero, Nuru Kabendera, mbali na kushukuru ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Kagera kuwapatia hati katika kipindi kifupi, alisema wamiliki wengi bado hawajui muda wa kuisha kwa hati na kutaka elimu ya uhuishaji kutolewa hadi yale maeneo ya vijijni ili wamiliki waweze kufahamu.

Naye mkazi wa kata ya Bakoba mtaa wa Nyakanyasi, Grace Kokuledi, aliwataka wamiliki wa ardhi kuwashirikisha watoto wao katika umiliki ardhi ili iwe rahisi kwao kuhuisha miliki pale itakapotokea Mungu amewachukua kwa kuwa hati hizo umiliki wake unafikia hadi miaka 99.




Mkuu wa Wilaya ya Moshi Mjini, Said Mtanda (katikati), baada ya kushuhudia utiaji saini wa ushirikiano kati ya Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) na Benki ya Ushirika Kilimanjaro (KCBL), wa kuwakopesha wakulima wa mkoa wa Kilimanjaro, kiasi cha Sh. bilioni 2 kupitia Mfuko Maalum wa Fedha kwa Wakulima Wadogo wa TADB, ili kuongeza tija. Kutoka (kushoto) ni Mwenyekiti wa Bodi ya Ushirika Kilimanjaro (KNCU), Cosmas Mushi, Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Frank Nyabundege, Meneja Mkuu wa KCBL, Godfrey Ng'urah na Ofisa Ushirika Kilimanjaro, Godbless Munuo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# RC ahimiza wataalamu ushirikishaji wananchi katika uhifadhi wa misitu

**Na Christina Haule,** LINDI

WATAALAMU wa misitu wametakiwa kuishirikisha jamii katika usimamizi shirikishi wa misitu (USM) ili kutunza misitu ambayo ni chanzo kikuu cha mvua na kuondokana na mabadiliko ya tabia nchi.

Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainab Telack, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kwamba wataalamu wa misitu hawana budi kuitumia vyema elimu yao waliyopata darasani sambamba na elimu za muda mfupi kupitia mashirika mbalimbali ya uhifadhi wa misitu.

Telack alisema kufanya hivyo kutasaidia kuboresha kilimo ambacho ndicho chanzo kikuu cha uchumi mkoani na nchini kwa ujumla.

Alisema kupitia misitu wanaweza kupata mvua na kuboresha zao la korosho, hivyo kutegemea kuvuna mazao yenye kuleta tija sambamba na kuajiri watu wengine na kupunguza ukosefu wa ajira, tatizo ambalo ni kubwa kwa sasa.

Kuhusu faida za uhifadhi misitu, Telack alisema mwaka 2020 waliuza korosho mkoani hapo na kupata Sh. bilioni 151 na mwaka huu wameshaanza kuuza korosho na kupata Sh. bilioni 71 na kwamba katika ufuta pia wamepata Sh. bilioni 121 kwa mwaka huu.

Alisema bila uhifadhi wa misitu mazao yakiwamo korosho na hayawezi kukua na kuleta tija kwa sababu mazao yoyote yanategemea mvua na kunyesha mvua kunategemea na utunzaji wa msitu uliopo.

Alisema amekuwa akiendelea kuwahamasha wananchi kujituma katika uhifadhi wa misitu na kilimo ili fedha nyingi zinazopatikana kwenye makundi zipatikane pia kwa mtu mmoja mmoja.

Pia aliwataka wakulima mkoani hapa kuacha kukata na kuchoma miti aina ya mipingo wanapoandaa mashamba na kwamba miti hiyo imeanza kutoweka katika maeneo hayo.

Alisema kupotea kwa miti hiyo kutaondoa uasili wa miti iliyopo nchini na kuharibu maana ya uhifadhi wenye faida kutokana na miti aina ya mipingo myeusi kuwa na soko kubwa nje ya nchi lakini pia inaweza kusababisha kutokuwa na vinyago vya kuonyesha uhalisia wa rasilimali za nchi.

Naye Ofisa kutoka Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA), Elida Fundi, alisema kwa sasa wanafundisha wataalamu wa misitu kutoka wilaya ya Kilolo, Liwale na Ruangwa ambako mradi wa kuhifadhi misitu kwa kuwezesha biashara endelevu ya mazao ya misitu Tanzania (CoForEST) upo kwa kuwapa elimu sahihi ya uhifadhi misitu.

Alisema wamekuwa wakiwapa elimu ya namna ya kutenga maeneo, kuyahifadhi na kufanya usimamizi shirikishi wa misitu kwa jamii (USMJ) na wao kusaidia kielimu vijiji vinavyozunguka kijiji husika ili kusaidia misitu isiweze kupotea.

# MORRISON AONYESHA UUNGWANA YANGA

Na Faustine Feliciane

WAKATI uongozi wa Klabu ya Yanga ukikubali hukumu ya rufani ya kesi dhidi ya mchezaji wa Simba, Bernard Morrison, kutoka Mahakama ya Usuluhishi ya Masuala ya Michezo (CAS), nyota huyo raia wa Ghana ameishukuru timu hiyo kwa kumpa nafasi ya kuichezea na kumtambulisha hapa nchini.

Juzi, CAS ilitoa hukumu ya kesi hiyo ya kimkataba na kumpa ushindi Morrison baada ya kubaini mkataba wa nyota huyo na Yanga uliisha tangu Julai 14, mwaka jana na hakukuwa na mkataba mwingine kama ambavyo Yanga walikuwa wanadai.

Lakini baada ya hukumu hiyo, Morrison alimwambia mwandishi wetu kwamba pamoja na mambo yote, suala hilo limekwisha na bado anatambua mchango wa Yanga kwake na anaamini kama si klabu hiyo basi asingefahamika hapa nchini.

"Nimeandika pia kwenye ukurasa wangu wa Instagram, sina ubaya na Yanga, haya masuala yalikuwa yakisheria na nashukuru Mungu yameisha, Yanga ndio walionitambulisha hapa nchini na mashabiki wake walinipokea na kunisapoti vizuri sana, nalitambua hilo na nawashukuru sana," alisema Morrison.

Alisema kwa sasa anaendelea na majukumu yake ndani ya klabu yake ya Simba na anafurahia kuwapo kwenye timu hiyo.

"Mambo mengine yanaendelea, akili yangu sasa naielekeza zaidi kwenye timu yangu na kwenye michezo iliyopo mbele yetu ili tuweze kufikia malengo ya klabu," aliongezea kusema Morrison.

Kwa upande wa Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Fredrick Mwakalebela, alisema wameipata hukumu ya CAS na wanakubaliana nayo ili mambo mengine yaendelee na jambo hili haliwezi kuwatoa kwenye malengo yao ya kutwaa ubingwa msimu huu.

"Tumepokea taarifa hiyo na hatuna kinyongo na hiyo hukumu, Yanga tutaendelea kupambania haki yetu kila tutakapoona tunastahili kufanya hivyo, kwa sasa mambo mengine yanaendelea na jambo hili haliwezi kututoa kwenye reli," alisema Mwakalebela.

Alisema kwa sasa timu imerejea kwenye mazoezi baada ya mapumziko ya siku mbili na wanajiandaa na mchezo wao wa Ligi Kuu dhidi ya Mbeya Kwanza utakaochezwa Jumanne ijayo katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya.

## Karafu Empire yaahidi kufanya kweli CANAF

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

TIMU ya Taifa ya Zanzibar ya Soka la Watu wenye Ulemavu 'Karafu Empire', imesema imejipanga kufanya vema katika michuano ya Mataifa ya Afrika kwa Walemavu (CANAF), inayotarajiwa kuanza kutimua vumbi Dar es Salaam kuanzia Ijumaa wiki hii hadi Desemba 5, mwaka huu.

Karafuu Empire ambayo imepangwa Kundi B pamoja na Angola, Kenya na Rwanda, inatarajia kuanza kutupa karata yake ya kwanza Jumamosi dhidi ya Angola, mchezo utakaopigwa katika Uwanja wa JK Park jijini Dar es Salaam.

Hata hivyo, Karafuu Empire, itakuwa na kibarua kigumu dhidi ya Angola ambayo ni nchi ya kwanza Afrika kuchukua Kombe la Dunia kwa Wenye Ulemavu.

Nchi nyingine zilizowahi kubeba ubingwa huo ni Urusi ambayo iliubeba mara nne mwaka 1998, 2002, 2003 na 2014 huku Brazil ikiutwaa mara tatu mwaka 2000, 2001 na 2005 kama ilivyo kwa Jamhuri ya Uzbekistan, mwaka 2007, 2010 na 2012.

Akizungumza na gazeti hili jana, Rais wa Shirikisho la Soka kwa Watu wenye Ulemavu wa Viungo Zanzibar, Hassan Haji 'Kificho', alisema maandalizi ya kuelekea michuano hiyo kwa Karafuu Empire yamekamilika na timu hiyo inatarajia kusafiri na wachezaji 12, viongozi saba pamoja na mkuu mmoja wa msafara.

Alisema wamepata mazoezi ya kutosha katika kujiandaa na michuano hiyo ya Afrika inayoshirikisha mataifa 15 ya Afrika.

Kificho alisema licha ya kukamilisha maandalizi kuelekea michuano hiyo, lakini timu hiyo imekosa msaada kutoka kwa wadau mbalimbali wa michezo hali iliyosababisha kuwapo kwa changamoto kubwa ya vifaa vya mazoezi.

"Wachezaji wamejiandaa, lakini tumekosa hamasa kutoka kwa wadau, hatukupata michango walau ya kututia moyo au hamasa ya kufika uwanjani hata pale tulipocheza michezo ya kirafiki," alisema huku akilipongeza Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), kwa misaada mbalimbali waliyotoa kwa ajili ya timu hiyo.

Katika mashindano hayo, ambayo Tanzania Bara itawakilishwa na Tembo Warriors, timu nane zitakazotinga robo fainali zitafuzu moja kwa moja Kombe la Dunia mwakani nchini Uturuki.

Hii inakuwa mara ya pili kwa Tanzania chini ya Shirikisho la Soka la Watu Wenye Ulemavu (TAFF), kuandaa mashindano makubwa, kwani ya kwanza yalikuwa ni ya Afrika Mashariki na timu ya Rwanda ilitwaa ubingwa na Kenya washindi wa pili, huku nafasi ya tatu ikichukuliwa na Tanzania na nafasi ya nne ikienda kwa Zanzibar. Ikumbukwe pia Tembo Warriors iliiwakilisha Tanzania katika Michuano ya Kombe la Mataifa Afrika yaliyofanyika Angola, Septemba 30 hadi Oktoba 14, mwaka 2019 na kushika nafasi ya nne.

Tembo Warriors ipo Kundi A pamoja na nchi za Sierra Lionne, Uganda na Morocco, wakati Kundi B likiundwa na Angola, Kenya, Rwanda na Zanzibar, Kundi C ipo Liberia, Cameroon, Gambia na Ethiopia na Kundi D ni Nigeria, Ghana na Misri.

**'OOOH YES!'...**




Kocha Mkuu wa Simba, Mhispania Pablo Franco, akimfuatilia mshambuliaji Meddie Kagere, katika mazoezi ya timu hiyo kujiandaa na mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Red Arrows ya Zambia itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumapili wiki hii. **MPIGAPICHA WETU**

## Machomane yalia joto chanzo vipigo Ligi Kuu

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

TIMU ya Machomane imesema hali ya hewa ya joto kali katika michezo iliyopita ya mzunguko wa kwanza hadi wa sita ndicho chanzo cha wao kufanya vibaya kwenye Ligi Kuu Zanzibar inayoendelea visiwani hapa.

Machomane ipo nafasi ya pili kutoka mkiani katika msimamo wa ligi hiyo ikiwa na alama moja baada ya kushuka dimbani mara sita na kuambulia sare moja huku ikipokea vipigo vitano.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa timu hiyo, Mohamed Kombo, alisema bado hawajapoteza matumaini ya kufanya vizuri katika ligi hiyo licha ya kupoteza michezo mitano.

**Alisema pamoja na mambo mengine, lakini sababu mojawapo ya wao kupoteza ni kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa kuwa joto kali sambamba na ratiba ya ligi hiyo kutokuwa rafiki hususan kwa mechi walizocheza majira ya saa nane mchana.**

Kombo alisema licha ya changamoto nyingine ya Kocha kutopata muda wa kutosha kuifundisha timu hiyo kutokana na matatizo ya kifamilia, lakini suala la michezo ya saa nane mchana ndio imeathili zaidi hasa katika kipindi hiki cha jua kali.

Aidha, alisema mchezo wake wa mzunguko wa saba dhidi ya Uhamiaji leo, watashuka dimbani wakiwa na lengo moja tu kupata alama zote tatu.

Ligi Kuu Zanzibar ambayo msimu huu inashirikisha timu 16, nne zitashuka daraja huku idadi kama hiyo zikipanda; mbili kutoka Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja na mbili kutoka Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Pemba.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ZIDANE KUTUA PSG
WACHEZAJI wa Klabu ya Paris St-Germain wanaamini kwamba Mauricio Pochettino ataondoka kuelekea Manchester United huku raia wa Ufaransa Zinedine Zidane akimrithi katika klabu ya PSG. **(Marca)**

### SALAH KUSAINI MKATABA
MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Mohamed Salah, anakaribia kusaini mkataba mpya wa muda mrefu katika klabu hiyo. Mchezaji huyo ataingia mwaka wa mwisho wa kandarasi yake msimu ujao huku klabu hiyo ikijiandaa kukamilisha masharti mapya ya mkataba wake. **(Team Talk)**

### SANCHEZ KUONDOKA LILLE
KIUNGO wa kati wa klabu ya Lille, Renato Sanches, amesema yuko tayari kuondoka klabuni hapo ili kupata changamoto mpya. **(L'Equipe)**

### BARCA, UMTITI KUACHANA
KLABU ya Barcelona huenda ikafuatilia mbali mkataba na mchezaji, Samuel Umtiti. Beki huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 28 ameshindwa kukubali pato lililopunguzwa kwa mshahara wake wa pauni 208,000 kwa wiki huku klabu hiyo ikikabiliwa na matatizo ya kifedha. **(Sport)**

### UNITED KULIPA EURO MIL. 10
MANCHESTER United italazimika kulipa euro milioni 10 iwapo wanataka kununua mkataba wa kocha raia wa Argentina, Mauricio Pochettino mwenye umri wa miaka 49 kutoka klabu ya PSG. **(Mirror)**

### LACAZETTE BASI TENA
ARSENAL haitajadili mkataba mpya na mshambuliaji wa Ufaransa, Alexandre Lacazette mwenye umri wa miaka 30, hadi mwishoni mwa msimu, licha ya kujua kwamba huenda wakampoteza mchezaji huyo kwa uhamisho wa bila malipo. Atletico Madrid, AC Milan, Marseille na Newcastle zote zinamnyatia mchezaji huyo. **(Sun)**

### LOPETEGUI AKANA UVUMI UTD
KOCHA wa Klabu ya Sevilla, Julen Lopetegui mwenye umri wa miaka 55, ameutaja uvumi unaomhusisha na klabu ya Manchester United kuwa mbaya. (Mirror)

### PEDRI ATAKIWA BAYERN
KLABU Bayern Munich inataka kumsajili mchezaji wa Barcelona mwenye umri wa miaka 18, Pedri licha ya kiungo huyo wa kati wa Hispania kuwa na kifungu cha euro bilioni moja katika mkataba wake kinachomzuia kuondoka. **(AS)**


### WOODWARD KUCHELEWA
MAKAMU Mwenyekiti wa Klabu ya Manchester United, Ed Woodward, anafikiria kuchelewesha kuondoka kwake katika klabu ya Old Tarfford ili kusaidia kumtafuta kocha mpya atakayemrithi Ole Gunnar Solskjaer. **(Sky Sports)**

### EMERY AMMULIKA MITROVIC
MSHAMBULIAJI wa Fulham, Aleksandar Mitrovic, anadaiwa kulengwa na klabu chungu nzima katika dirisha la uhamisho la Januari, huku kocha wa klabu ya Villareal, Unai Emery akitarajiwa kumsaini mshambuliaji huyo. **(Mirror)**

### BRUCE KUINOA UNITED
ALIYEKUWA kocha wa Newcastle, Steve Bruce, anadaiwa kuwa tayari kuchukua uongozi wa muda mfupi katika klabu ya Manchester United. Raia huyo mwenye umri wa miaka 60, aliiwakilisha Man United zaidi ya mara 300 akiwa mchezaji. **(The Athletic)**

### HLOZEK ATAKIWA WEST HAM
KLABU ya West Ham wanafanya bidii kumsaini mshambuliaji wa Sparta Prague na Jamhuri ya Czech, Adam Hlozek mwenye umri wa 19. **(Football Insider)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO SASA AMTAKA ENRIQUE KUINOA UNITED

**Mbali na Zidane, makocha wengine wanaotajwa ni Erik ten Hag wa Ajax, Pochettino wa PSG na Rodgers wa Leicester, lakini...**

**MANCHESTER, England**

WAKATI dunia ikiamini kuwa Manchester United inafanya mipango ya kumpa ajira Zinedine Zidane kuwa kocha wa timu hiyo, inadaiwa nyota wa timu, Cristiano Ronaldo anapendekeza jina la kocha mwingine kabisa.

Nyota huyo wa kimataifa wa Ureno, Ronaldo amempendekeza Luis Enrique ambaye amewahi kuwa kocha wa Barcelona.

Ronaldo anataka Enrique ndiye awe mrithi wa Ole Gunnar Solskjaer badala ya Zidane ambaye wamewahi kufanya naye kazi kwa mafanikio makubwa kule Real Madrid.

Makocha wengine wanaotajwa kuwa wanaweza kupata nafasi ya kuinoa Man United ni Erik ten Hag wa Ajax, Mauricio Pochettino wa Paris Saint-Germain na Brendan Rodgers wa Leicester City.

Enrique amekuwa akiinoa Hispania tangu mwaka 2019, kocha huyo mwenye umri wa miaka 51, aliifundisha Barcelona kwa mafanikio makubwa akibeba LaLiga mara mbili na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 710

MECHI KALI
HOME
MANCHESTER CITY
1.67 | 4.10 | 4.58
PARIS ST GERMAIN
AWAY

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# PEPE AINGIA RADA ZA MILAN

**MILAN, Italia**

KLABU ya AC Milan imeripotiwa kuingia kwenye orodha ya klabu zinazowania saini ya mshambuliaji wa Arsenal, Nicolas Pepe.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ivory Coast, amekuwa na wakati mgumu kuendana na thamani ya bei yake ya pauni milioni 72 tangu awasili miaka miwili iliyopita na amepoteza ushawishi kwa Mikel Arteta.

Pepe anatajwa kuwa atamaliza kibarua chake na Arsenal mwaka 2022, huku "Washikabunduki' hao wakidaiwa kuwa tayari kupunguza hasara na kumuuza kwa kitita cha pauni milioni 25.

Crystal Palace wanadaiwa kuweka mipango ya kuingia windoni kumnunua Pepe, lakini Milanista imeripoti kwamba, Milan wanatumaini kuingia mazima kwenye dili na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 katika dirisha la uhamisho la Januari.

Ripoti hiyo inaongeza kuwa bosi wa Rossoneri hao, Stefano Pioli ni shabiki mkubwa wa mchezaji huyo wa zamani wa Lille, mwenye uwezo huku Arsenal wakionekana kutokuona mchango wake.

Mshambuliaji huyo amefanikiwa kuweka nyavuni mabao 25 na asisti 18 katika mechi 98 alizowachezea 'Washikabundi hao, lakini ameanza kwenye mechi moja tu kati ya sita za mwisho za Ligi Kuu ya Uingereza.

# Ramsey agombewa England



**LONDON, England**

NYOTA wa Juventus, Aaron Ramsey, anajiandaa kumaliza mkataba wake na klabu ya Juventus na kurejea katika Ligi Kuu England na amekuwa na wakati mgumu huko Turin tangu ajiunge na klabu hiyo ya Serie A mwaka 2019 kama mchezaji huru.

Na klabu zilizoonyesha kumtaka kiungo huyo ni Arsenal, Newcastle na Tottenham lakini 'Washikabunduki' huenda wakashinda katika kinyang'anyiro hicho kwa mchezaji wao wa zamani.

Mikel Arteta anajaribu kuijenga timu ya vijana yenye nguvu lakini pia anahitaji vichwa vyenye uzoefu kama Ramsey ambaye anaijua vizuri Arsenal.

Spurs ambao ni mahasimu wakubwa wa Arsenal, pia wameonyesha nia ya kuipata saini ya kiungo huyo lakini, je, mashabiki wa Spurs watampokea? Kwani Ramsey aliwahi kukataa kujiunga na Tottenham na alipoulizwa mwaka 2018 kama angeweza kuhamia Spurs alijibu hapana.

Matajiri wapya wa EPL Newcastle wanataka majina makubwa sasa kwenye timu yao kwani wanao uwezo wa kumudu mishahara mikubwa, hii inamaanisha Ramsey anaweza kwenda Newcastle.

## HABARI MICHEZO


,494,580

# JACKPOT

## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 27/11/21 | 18:00 | Crystal Palace vs Aston Villa | 2.18 | 3.30 | 3.35 |
| 02. 27/11/21 | 18:00 | Hull City vs Millwall | 2.70 | 3.09 | 2.60 |
| 03. 27/11/21 | 18:00 | Huddersfield vs Middlesbrough | 2.46 | 3.10 | 2.85 |
| 04. 27/11/21 | 20:00 | Juventus vs Atalanta | 2.22 | 3.46 | 3.12 |
| 05. 27/11/21 | 20:30 | Mallorca vs Getafe | 2.43 | 2.90 | 3.30 |
| 06. 27/11/21 | 20:30 | Cercle Brugge vs Mechelen | 2.66 | 3.45 | 2.44 |
| 07. 27/11/21 | 20:45 | Fortuna Sittard vs Groningen | 2.72 | 3.26 | 2.47 |
| 08. 27/11/21 | 23:00 | Villarreal vs Barcelona | 2.69 | 3.33 | 2.57 |
| 09. 28/11/21 | 15:30 | Nurnberg vs St. Pauli | 2.60 | 3.23 | 2.60 |
| 10. 28/11/21 | 17:00 | Brentford vs Everton | 2.38 | 3.20 | 3.05 |
| 11. 28/11/21 | 17:00 | Bordeaux vs Brest | 2.42 | 3.34 | 2.84 |
| 12. 28/11/21 | 18:15 | Espanyol vs Real Sociedad | 3.30 | 3.25 | 2.22 |
| 13. 28/11/21 | 18:30 | Maritimo vs Pacos Ferreira | 2.66 | 3.10 | 2.66 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE

"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATANO - 24 - NOVEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1748 | Jeonnam Dragons vs Daegu | 3.09 | 3.09 | 2.21 |
| 14:00 | 4144 | Persebaya Surabaya vs Persita Tangerang | 1.77 | 3.48 | 4.06 |
| 14:30 | 1972 | Havadar vs Aluminium Arak | 3.17 | 2.50 | 2.60 |
| 15:00 | 1796 | KF Gjilani vs KF Drita | 2.35 | 3.10 | 3.20 |
| 15:00 | 3665 | KF Drenica Skenderaj vs KF Llapi | 2.94 | 2.89 | 2.41 |
| 15:00 | 3836 | Sidama Bunna SC vs Sebeta City FC | 3.10 | 2.95 | 2.28 |
| 15:00 | 5745 | FC Minaj vs Kolos Kovalivka | 2.89 | 3.18 | 2.27 |
| 15:00 | 5941 | Dorogi FC vs Szolnoki Mav | 2.65 | 3.10 | 2.80 |
| 15:30 | 1758 | Varnsdorf vs Opava | 2.30 | 3.32 | 2.74 |
| 15:30 | 3317 | NK Drava Ptuj vs Krka | 7.50 | 5.58 | 1.27 |
| 15:35 | 3998 | AL Ain vs Al Wehda | 2.98 | 3.08 | 2.27 |
| 15:40 | 1438 | Bahla vs Saham Club | 2.03 | 3.25 | 3.85 |
| 16:00 | 2189 | Crewe U23 vs Sheffield Wednesday U23 | 2.35 | 3.46 | 2.59 |
| 16:00 | 3909 | Prison Leopards vs Zesco United | 4.34 | 2.85 | 1.93 |
| 16:00 | 4220 | Konkola Blades vs Nkana FC | 2.71 | 2.76 | 2.71 |
| 16:00 | 4581 | Musanze vs Espoir FC | 3.24 | 3.43 | 2.00 |
| 17:00 | 1192 | Radnik Surduluca vs Backa Topola | 3.30 | 3.55 | 2.10 |
| 18:00 | 2356 | Tshakhuma vs Maritzburg Utd | 2.84 | 2.80 | 2.70 |
| 18:00 | 5952 | Mekelakeya vs Saint George FC | 3.94 | 2.89 | 2.00 |
| 18:15 | 4885 | Jeddah Club vs Al Orubah | 2.17 | 3.13 | 3.13 |
| 18:30 | 1128 | Stellenbosch vs Orlando Pirates | 2.95 | 2.85 | 2.56 |
| 18:30 | 2206 | Kaizer Chiefs vs Amazulu | 2.28 | 2.83 | 3.47 |
| 18:30 | 2934 | Mamelodi Sundowns vs SuperSport Utd | 1.74 | 3.64 | 4.33 |
| 18:30 | 4038 | Spartak Moscow vs Napoli | 5.20 | 4.20 | 1.59 |
| 19:00 | 1564 | MFK Karvina vs Banik Ostrava | 3.95 | 3.60 | 1.89 |
| 19:00 | 2062 | Banga Gargzdai vs Kedainiai Nevezis | 1.49 | 4.40 | 6.20 |
| 19:05 | 1583 | Al Nasr Salalah vs AL Musanaa | 1.95 | 3.13 | 3.76 |
| 20:00 | 2137 | Zalgiris vs FK Panevezys | 1.62 | 3.97 | 4.36 |
| 20:00 | 4245 | Zaglebie Sosnowiec vs Chrobry Glogow | 2.14 | 3.24 | 3.09 |
| 20:15 | 1597 | MAS Maghrib A Fes vs FAR Rabat | 2.65 | 2.74 | 2.79 |
| 20:30 | 2516 | St. Pauli vs Sandhausen | 1.35 | 5.08 | 7.04 |
| 20:45 | 2985 | Inter vs Shakhtar Donetsk | 1.30 | 5.61 | 8.81 |
| 20:45 | 3951 | Besiktas vs Ajax | 6.40 | 4.90 | 1.43 |
| 22:15 | 1417 | Caracas FC vs Estudiantes FC | 2.31 | 3.20 | 3.20 |
| 22:30 | 1893 | FUS Rabat vs Difaa El Jadidi | 2.03 | 2.90 | 3.82 |
| 22:30 | 3051 | Korona Kielce vs GKS Tychy | 2.02 | 3.28 | 3.33 |
| 22:45 | 2742 | Fulham vs Derby | 1.28 | 5.27 | 9.18 |
| 22:45 | 4188 | Blackburn vs Peterborough | 1.65 | 3.74 | 4.82 |
| 22:45 | 4241 | QPR vs Huddersfield | 1.96 | 3.43 | 3.58 |
| 22:45 | 4302 | Millwall vs Bournemouth | 3.29 | 3.29 | 2.12 |
| 22:45 | 4870 | Cardiff vs Hull City | 2.06 | 3.29 | 3.44 |
| 22:45 | 5848 | Barnsley vs Swansea | 2.90 | 3.19 | 2.37 |
| 22:45 | 5945 | Ross County vs Hibernian | 3.07 | 3.36 | 2.22 |
| 22:45 | 5976 | Bristol City vs Stoke City | 3.23 | 3.28 | 2.15 |
| 23:00 | 1479 | Sporting Lisbon vs Borussia Dortmund | 2.65 | 3.45 | 2.55 |
| 23:00 | 2056 | Sheriff Tiraspol vs Real Madrid | 9.83 | 5.90 | 1.27 |
| 23:00 | 4250 | Atletico Madrid vs AC Milan | 1.66 | 3.95 | 4.90 |
| 23:00 | 4780 | Liverpool vs Porto | 1.88 | 3.76 | 3.81 |
| 23:00 | 5727 | Brugge vs RB Leipzig | 3.31 | 3.66 | 2.06 |
| 23:00 | 5826 | Manchester City vs Paris St Germain | 1.67 | 4.10 | 4.58 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.




# SOUTHGATE ASAINI MKATABA MPYA

**LONDON, England**

KOCHA wa Timu ya Taifa ya England, Gareth Southgate, ameongeza mkataba mpya wa kuinoa timu hiyo hadi mwaka 2024.

Southgate alikuwa akiutumikia mkataba wa kuiongoza timu hiyo ambao ungefikia tamati baada ya michuano ya Kombe la Dunia 2022.

Baada ya hatua chanya zinazopigwa na timu hiyo, ni dhahiri Southgate anastahili mkataba mpya.

Southgate ameiongoza England kwenye fainali ya Euro 2020 bila kupoteza mchezo wowote (ukiacha fainali) na ameendelea kufanya vizuri zaidi baada ya kuivusha timu hiyo na sasa, England ni miongoni mwa timu za awali kufuzu Kombe la Dunia 2022.

Huu ni mwendelezo wa Southgate kuendelea kukinoa kikosi cha timu ya Taifa cha England ambapo alianza kazi hiyo mwaka 2016.

# Pedri ashinda tuzo ya Golden Boy



**BARCELONA, Hispania**

KIUNGO wa Barcelona, Pedri ametajwa kuwa mshindi wa tuzo ya Golden Boy kwa mwaka 2021 na kumbwaga Jude Bellingham wa Borussia Dortmund.

Pedri mwenye umri wa miaka 18, anakuwa mchezaji wa pili wa Barca kushinda tuzo hiyo tangu aliposhinda Lionel Messi mwaka 2005.

Pedri alifurahia msimu tangu alipojiunga na Barcelona akitokea klabu ya Las Palmas mwaka 2020 majira ya joto.

Na alikuwa mchezaji tegemeo kwa Barca na timu ya Taifa ya Hispania akifanikiwa kutwaa mataji ya Kombe la Mfalme (Cop del Rey) na kuvaa medali ya silva kwenye michuano ya Olympic ya Tokyo.

Pedri anafuata nyayo za Erling Haaland, Joao Felix na Matthijs de Ligt ambao wameweza kushinda kama wachezaji bora wa chini ya umri wa miaka 21 kwa misimu ya hivi karibuni.

"Nawashukuru Tuttosport kwa tuzo hii ambayo inanifanya nijivunie. Asante pia kwa washiriki wote na mashabiki ambao wamekuwa wakiniunga mkono kila wakati katika mwaka 2021 hii nzuri kwangu," alisema.

"Na bila shaka, shukrani nyingi kwa Barca, timu ya taifa, familia yangu, marafiki zangu na bila shaka kwa wale wote ambao wamekuwa karibu nami siku baada ya siku ambao bila ya wao nisingeweza kushinda Golden Boy."

# Michezo

Jumatano Novemba 24, 2021

Nipashe



Ronaldo sasa amtaka Enrique kuinoa United

UKURASA 21

IMENOGA TENA...




Makamu wa Kwanza wa Rais TFF, Athuman Nyamlani (kulia) na Mkurugenzi wa Uwekezaji GSM Group, Injinia Hersi Said wakionyesha mfano wa hundi ya mkataba wa udhamini mwenza wa Ligi Kuu ya NBC wenye thamani ya Sh. bilioni 2.1 kwa miaka miwili, Dar es Salaam jana. **MPIGAPICHA WETU**

# SIMBA, YANGA MAMBO MAGUMU ZAIDI LIGI KUU

- Licha ya kulia kukamiwa, mabilioni tena yaongezwa ushindani ubingwa Bara huku...

**Na Saada Akida**

LICHA ya miamba ya soka nchini Simba na Yanga, awali kukiri kwamba msimu huu zimekuwa zikikamiwa zaidi kutokana na wadhamini wa Ligi Kuu kumwaga ukwasi mkubwa, hivyo kila timu kuwania nafasi za juu ili kunufaika na dau kubwa mwishoni mwa msimu, hali hiyo sasa huenda ikaongezeka zaidi baada ya mabilioni zaidi kuongezewa katika kinyang'anyiro hicho.

Hiyo ni baada ya Shirikisho la Soka nchini (TFF) na GSM Group of Companies kusaini mkataba wa miaka miwili wenye thamani ya Sh. bilioni 2.1, kuwa mdhamini mwenza wa uendeshaji wa ligi hiyo ya NBC Premier League.

Tayari TFF ilishaingia mkataba na Kampuni ya Azam Media Limited wa haki ya matangazo ya televisheni wenye thamani ya bilioni 225.6 za Kitanzania kwa kipindi cha miaka 10, lakini pia ilisaini mkataba mwingine wa miaka 10 wa haki ya matangazo ya redio na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) wenye thamani ya Sh. bilioni 3.54.

Mbali na udhamini huo wa haki za matangazo kutoka Azam Media na TBC, TFF iliingia pia mkataba wa miaka mitatu na Benki ya NBC kuwa mdhamini mkuu wa ligi hiyo wenye thamani zaidi ya Sh. bilioni 2.5 bila kodi ya ongezeko la thamani (VAT).

Hata hivyo, udhamini wa Azam Media ndio ulioongeza ushindani zaidi baada ya kuongeza thamani ya Ligi Kuu kwa kutangaza bingwa atapata bonasi ya Sh. milioni 500, mshindi wa pili akipata milioni 250, wa tatu milioni 225 na wa nne akipata milioni 200, zawadi hizo zitaongezeka kila mwaka na kila timu itapata bonasi kulingana na nafasi iliyopo hadi ile itakayoburuza mkia, jambo ambalo limeongeza ushindani.

Lakini pia, katika mkataba huo klabu za Ligi Kuu zitakuwa na malipo makubwa kila mwezi ambapo kila timu itapata mgawo wa kiasi cha Sh. milioni 40 kwa ajili ya kulipa mishahara ya wachezaji.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana katika hafla ya makubaliano ya mkataba huo na GSM, Makamu wa Pili wa Rais wa TFF, Athumani Nyamlani, alisema fedha hizo za udhamini zitatumika kwa manufaa ya klabu na timu zinazoshiriki Ligi Kuu.

"Ligi ya Tanzania imekuwa bora ikiwamo barani Afrika, na kwa ubora huu, tunatarajia wadhamini wengine kujitokeza kuendelea kuipa thamani ligi yetu," alisema.

Nyamlani alisema Sh. bilioni 2.1 ni kiasi kikubwa cha fedha kwa sababu miaka ya nyuma baadhi ya timu zilikuwa zinapata shida ya safari ya kwenda katika vituo kucheza mechi na hata kukaa kwa miezi sita na kuendelea bila kulipwa mishahara, lakini kwa udhamini huo tatizo hilo litamalizika.

Alisema fedha hizo zitaenda kwa walengwa kwa makubaliano ya mdhamini na kwamba wataweka mfumo maalum kuratibu matumizi ya fedha zote kwa kila klabu ambazo zinatolewa na wadhamini.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Uwekezaji wa GSM, Injinia Hersi Said, alisema wameingia mkataba huo wenye thamani ya Sh. bilioni 2.1 ili kuongeza nguvu kwa timu za soka hapa nchini.

"Hatuwezi kuwa na timu ya taifa bora kama hatuna klabu ambazo haziko imara kifedha na hili tumeliona na ndio maana tumeona ni vema kuongeza nguvu katika jitihada za kusaidia soka hapa nchini.

"TFF ya sasa ni imara na salama, tumeona busara na imani yetu kufanya nao kazi kwa kuingia makubaliano ya udhamini mwenza wa Ligi Kuu Tanzania Bara," alisema Hersi.

## Morrison aonyesha uungwana Yanga



**Na Faustine Feliciane**

WAKATI uongozi wa Klabu ya Yanga ukikubali hukumu ya rufani ya kesi dhidi ya mchezaji wa Simba, Bernard Morrison, kutoka Mahakama ya Usuluhishi ya Masuala ya Michezo (CAS), nyota huyo raia wa Ghana ameishukuru timu hiyo kwa kumpa nafasi ya kuichezea na kumtambulisha hapa nchini.

UK. 20

## Ramsey agombewa na miamba England



**LONDON, England**

NYOTA wa Juventus, Aaron Ramsey, anajiandaa kumaliza mkataba wake na klabu ya Juventus na kurejea katika Ligi Kuu England na amekuwa na wakati mgumu huko Turin tangu ajiunge na klabu hiyo ya Serie A mwaka 2019 kama mchezaji huru.

Na Klabu zilizoonyesha kumtaka kiungo huyo ni Arsenal, Newcastle na Tottenham lakini 'Washikabunduki' huenda wakashinda katika kinyang'anyiro hicho kwa mchezaji wao wa zamani.

UK. 22

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >